Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo



Uk. 24

**Stars inawezekana**

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00047 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Januari 17 - 23, 2024 |

## Tumeyamaliza, ATCL ruksa kubeba mizigo Kenya




Uk. 3

## Konokono wazua sintofahamu mashamba ya kahawa Mbozi



Uk. 5



Uk.23

### WANAFUNZI KUCHELEWA KURIPOTI:

# Ma-RC, DC wacharuka

- Wavalia njuga jitihada za Rais Samia
- Wapita shule moja hadi nyingine kukagua
- Mgambo waagizwa kutinga nyumba kwa nyumba





Uk. 3

## Mnyeti awatolea uvivu madaktari wa mifugo

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Ikulu Tunguu, Zanzibar jana.





Uk. 7

## Tanga Mpo? Mjiandae, Makonda huyo Jan 20



Uk. 5

## Shanga yatolewa kwenye mapafu ya mtoto MNH

CAF AFRICA CUP OF NATIONS CÔTE D'IVOIRE 23

## Matokeo/ Ratiba Michuano ya AFCON 2023

Uk. 24

# Tz, Angola zasaini hati 3 za ushirikiano

## ■ Ni katika mafuta, gesi, visa, afya

**Na Mwandishi**

TANZANIA na Angola, zimesaini hati tatu za Makubaliano ya Ushirikiano (MoUs) katika sekta ya mafuta na gesi, kuondoleana visa kwa wenye hati/pasi za kusafiria za kidiplomasia na za kikazi pamoja na ushirikiano katika sekta ya afya.

Makubaliano hayo yalisainiwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Balozi Téte António wakati wa Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Angola uliomalizika jana Zanzibar.

Waziri Makamba alisaini hati mbili za makubaliano ya ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi na kuondoleana visa/pasi kwa wenye hati za kusafiria za kidiplomasia na za kikazi.

Aidha, Waziri Ummy alisaini hati ya ushirikiano katika sekta ya afya.

Mara baada ya kusainiwa kwa hati hizo, Waziri Makamba alisema Tanzania na Angola zina uhusiano wa kihistoria ulioanzishwa na viongozi wakuu wa kitaifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Agostino Neto.

Alisema walianzisha uhusiano huo kwa matarajio kuwa utoe manufaa kwa nchi zote mbili.

Pamoja na mambo mengine, katika mkutano huo, viongozi hao walijadili masuala mbalimbali ya uhusiano wa kisiasa, ulinzi, elimu, afya, mafuta na gesi, uchumi wa buluu, usafiri wa anga, kubadilishana visa, kusafiri bila visa kati ya nchi zetu mbili na hatimaye wakaingia makubaliano ya ushirikiano.

Kadhalika, viongozi hao walikubaliana kuyafanyia kazi masuala mbalimbali husasan, uwepo wa ndege za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam hadi Luanda pamoja na kufanya kongamano la biashara na uwekezaji na kuziwezesha sekta binafsi kufanya kazi kwa pamoja na ushirikiano zaidi.

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Balozi António alisema Angola imefurahishwa na uamuzi wa Serikali ya Tanzania kukubali kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) na kuelezea utayari wake wa kushirikiana katika nyanja walizokubaliana kwa maslahi ya pande zote mbili.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba.

**Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Balozi António alisema Angola imefurahishwa na uamuzi wa Serikali ya Tanzania kukubali kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Pili.**



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

# Jela kwa kuharibu mali ya kanisa ya mil. 48/-

**Na Mwandishi Wetu, Geita**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Geita, imemhukumu mkazi wa Mtaa wa Katundu wilayani Geita, Elpidius Edward, kifungo cha miaka mitatu jela baada ya kumvamia Kanisa Kuu la Kiaskofu la Jimbo Katoliki Geita na kuharibu mali zenye thamani ya Sh. milioni 48.2.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na mahakama hiyo baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa dhidi yake.

Kabla ya kutiwa hatiani, Edward alidaiwa kufanya uharibifu huo ndani ya kanisa saa 8:00 usiku Februari 26, mwaka jana.



# Ruwasa yapewa siku 14 kuzuia upotevu wa maji

**Na Mwandishi Wetu, Mufindi**

MKUU wa Wilaya ya Mufindi, Dk. Linda Salekwa, ametoa siku 14 kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kuzuia upotevu wa maji, kufuatia tangi la kuhifadhi maji katika Kijiji cha Kitelewasi, wilayani humo kuvujisha maji.

Alitoa agizo hilo jana baada ya Kamati ya Siasa ya Wilaya kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo, ukiwemo mradi huo wa Ugute–Kitelewasi.

Alisema haiwezekani kuacha maji yakiendelea kumwagika, wakati wataalam hao wanajua njia ya kutatua changamoto hiyo.

“Hii si sawa kwa sababu maji mengi yanapotea wakati tumewazuia wananchi kuyatumia maji hayo kwa kilimo, hii ni roho mbaya kama zilivyo roho mbaya nyingine,” alisema Dk. Salekwa.

Aidha, Dk. Salekwa alisema Ruwasa wanapaswa kuhakikisha wanaweka kizuio “ball valve” ili maji hayo yasiendelee kupotea bila sababu za msingi.

Hata hivyo, aliishukuru kamati hiyo kwa namna ambavyo wametembelea mradi huo, wakianzia kwenye chanzo na hatimaye kufika katika tangi hilo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM wilaya hiyo, George Kavenuke, alisema mradi huo utasaidia wananchi wa maeneo hayo kwa kuwa kipindi cha nyuma walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

“Mradi huu ni msaada mkubwa kwa wananchi wa maeneo haya kwa sababu walikuwa wanafuata huduma hii mbali na kupoteza muda mwingi kuchota maji porini na kukutana na changamoto mbalimbali,” alisema.

Awali, akisoma taarifa ya mradi huo kwa niaba ya Meneja wa Ruwasa, Happy Mrisho, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Ruwasa, Venancia Kihwelo, alisema mradi huo unatarajia kuhudumia vijiji vya Ugute na Kitelewasi ambapo jumla ya wananchi 3,497 watanufaika.

Alisema mradi huo unatekelezwa kupitia fedha za Mfuko wa Maji wa Taifa na gharama za ujenzi wa mradi huo ni Sh. bilioni 1.6 hadi kukamilika kwake.

Akijibu maagizo ya Mkuu wa Wilaya, ofisa huyo alisema wamepokea maelekezo hayo na kwamba watayafanyia kazi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi za Watumiaji Maji, Aloice Lulandala, alisema: “Baada ya mradi huu kufika kijijini kwetu, utakuwa mkombozi mkubwa kwa sababu tulikuwa tunawapa adhabu kubwa kufuata huduma hiyo mbali na maeneo yetu.”



Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Dk. Linda Salekwa.

# Wauguzi na wakunga 1,330 wafutiwa matokeo ya mitihani

**Na Godfrey Sanga**

BARAZA la Ukunga na Uuguzi Tanzania, limetangaza kufuta matokeo ya mitihani wa usajili na leseni za wauguzi na wakunga kwa watahiniwa wa 1,330 wa ngazi ya stashahada 1,330 uliofanyika Septemba 7, mwaka jana.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Afya kupitia mtandao wake wa kijamii wa Instagram ilisema baraza hilo limefikia hatua hiyo baada ya kubaini kulikuwepo na vitendo vya kuvuja kwa mitihani hiyo katika ngazi ya stashahada.

Ilisema mtuhumiwa aliyehusika na uvujaji huo, tayari amebainika na amesimamishwa kazi ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Aidha, kufuatia hatua hiyo, baraza hilo limesema watahiniwa watapewa nafasi ya kufanya mtihani mwingine bila malipo

utakaofanyika Februari 16, mwaka huu mkoani Dodoma.

Jumla ya wauguzi na wakunga 1,434 kwa ngazi zote astashahada (44), stashahada (1,330), na shahada (60), walifanya mtihani huo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma.

# Mnyeti awatolea uvivu madaktari wa mifugo



**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

NAIBU Waziri wa Mifugo, Alexander Mnyeti, amewataka madaktari na maafisa Mifugo, kufanya kazi walizosomea na kuwatembelea wafugaji badala ya kuwa wakusanya mapato wa halmashauri.

Alitoa wito huo jijini Dodoma juzi wakati akizindua Baraza la Veterinari Tanzania awamu ya sita baada ya baraza hilo kupata wajumbe.

"Maafisa mifugo kwenye halmashauri, wanajifanya watumishi wa halmashauri wa kukusanya mapato kwenye minada, kukusanya ushuru wa ng'ombe badala ya kufanya kazi za udaktari na kuwatembelea wafugaji," alisema.

Alisema baadhi ya maafisa mifugo, wamekuwa wakijikita zaidi kukusanya mapato ya halmashauri minadani na kuacha kuwatembelea wafugaji kujua matatizo yao.

Aidha,
alilitaka baraza hilo kuhakikisha linachukua hatua zaidi kwa maafisa mifugo ambao wamekuwa wakifanya kazi kinyume cha maadili pamoja na kuwapatia semina mara kwa mara kuwakumbusha wajibu wao kwa wananchi.

Alisema ifike wakati maafisa mifugo wanaokiuka maadili wafukuzwe kazi pamoja na kufutiwa leseni zao kazi hiyo ifanywe na watu watakaofuata taratibu na maadili ya kazi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe, alisema ana imani maafisa mifugo waliokuwa wakituma maombi kusajiliwa kwenye Baraza la Veterinari Tanzania sasa wataanza kusajiliwa rasmi kwa kuwa baraza hilo tayari limezinduliwa.

Alifafanua kuwa amekuwa akipata ujumbe kwa njia ya simu kutoka kwa baadhi ya maafisa mifugo ambao wamekuwa wakihitaji kusajiliwa, lakini hawakusajiliwa kwa kuwa Baraza halikuwa na wajumbe.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Veterinari Tanzania, Profesa Lughano Kusiluka, alisema Baraza limekuwa likisimamia sheria za veterinari kwa kuhakikisha wataalamu wanaohusika na kutoa huduma za afya za wanyama wafugwao na wasiofugwa, wanafanya kazi kwa kufuata sheria na maadili.

Alisema kazi kubwa ya Baraza ni kuwaandikisha na kuwaingiza kwenye daftari la baraza hilo na kufuatilia kiwango na huduma wanazotoa, kusimamia elimu ya wanyama inayotolewa na taasisi mbalimbali na kufuatilia kwa ukaribu wadau wapate huduma inayotakiwa.

# Aweso amtwisha zigo Katibu Mkuu wake

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amemtaka Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Jamali Katundu, kuweka mkazo maalum katika eneo la uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa.

Aidha, amemtaka kufanya tathmini ya utendaji wa magari ya uchimbaji visima, hususani, eneo la ufanisi na gharama za uchimbaji visima hivyo.

Aliyasema hayo juzi jijini Dodoma wakati wa kikao maalum cha tathmini ya utendaji wa wizara yake kwa mwaka 2024 ambapo pamoja na mambo mengine, msisitizo mkubwa umewekwa katika eneo la uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa.

"Tathmini ya kina ifanyike na mchakato wa kutengeneza mfumo ambao utakuwa na misingi bora ya utendaji uanze mara moja," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Waziri Aweso alisema mafanikio yaliyopatikana mwaka jana, yako wazi kwa kila mwananchi, lakini yako maeneo ambayo wizara haikufanya vizuri hivyo ni wajibu watendaji kuhakikisha wanarekebisha pale ambapo mambo hayakwenda vizuri.



# Tumeyamaliza, ATCL sasa ruksa kubeba mizigo Kenya

**Na Mwandishi Wetu, Dar**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imeruhusu tena vibali vya Shirika la Ndege la Kenya (KQ) vya kuendesha safari za ndege za abiria kati ya Nairobi na Dar es Salaam chini ya vifungu vya Haki za Uhuru wa Trafiki namba tati na nne na imetengua uamuzi wake iliyotoa mwanzoni mwa wiki.

Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari jana alisema wametoa ruhusa hiyo baada ya uamuzi wa Mamlaka ya Anga ya Jamhuri ya Kenya kukubali ombi la Tanzania la Kenya kusafirisha mizigo yao yote kwa kutumia Kampuni ya Air Tanzania kuanzia jana kwa kuzingatia Haki za Trafiki nambari tano kati ya Nairobi na Nchi za dunia ya tatu.

Ikumbukwe kuwa mwanzoni mwa wiki hii baada ya TCAA kutangaza zuio la KQ kutua Tanzania, saa chache baadaye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba alinukuliwa akisema amefanya mazungumzo na Waziri mwenzake anayeshughulikia masuala ya kigeni Nchini Kenya, Musalia Mudavadi na tayari wamekubaliana kumaliza sakata hilo ndani ya siku tatu.

# RC: Ajenda kupunguza vifo vya mama na mtoto

**Na Mwandishi Wizara ya Afya, Dodoma**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema sekta ya afya itaendelea kuweka kipaumbele ajenda ya kupunguza vifo vya mama na mtoto katika vikao vinavyofanyika ngazi zote za mkoa ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi ikiwa ni malengo ya Taifa na dunia.

Aliyasema hayo jijini Dodoma juzi wakati akifungua kikao kazi chenye lengo la kujadili mikakati ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, mama na watoto.

"Kupunguza vifo vya mama na mtoto, ni malengo ya dunia, lakini pia ni dhamira yake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, hivyo, sisi watendaji wake ni lazima tupambane nayo kwa kumuunga mkono Rais na dunia kwa ujumla," alisema.

Alisema, ni vyema Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji awe anashiriki vikao vya kikanuni katika ngazi zote za halmashauri ili atoe taarifa ya hali ilivyo juu ya vifo vinavyotokea pamoja na changamoto zake.

"Kama kuna mama mjamzito ambaye hafiki katika vituo vya kutolea huduma za afya tupate taarifa ili watendaji wa wilaya na kijiji wazidi kutoa rai na kuelimisha kupitia mikutano yao ya hadhara kwa wananchi," alisema.

Aidha, aliwataka waganga wakuu wa wilaya, kupeleka taarifa za wilaya juu ya vifo vya mama na mtoto kila wiki katika ofisi za wakuu wa wilaya ili kuwa na mkakati wa pamoja wa kuondoa vifo visivyo na ulazima kwa kushirikiana na wataalamu.

Katika hatua nyingine, alisema Serikali imedhamiria kupunguza tatizo la kansa ya kizazi kwa wanawake, ambapo aliwataka wajitokeze kupima ili wapate matibabu haraka kwa kuwa huduma hiyo inatolewa bila malipo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Idara ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto, Dk. Ahmad Makuwani, alisema Wizara ya Afya imeongeza kiwango cha watumiaji wa vituo vya afya wakati wa kujifungua na kufikia asilimia 81 ambapo mwaka 2016 vilikuwa asilimia 63.

## WANAFUNZI KUCHELEWA KURIPOTI:

# Ma-RC, DC wacharuka



> Agizo la DC Ngoma, Ofisa Miradi kutoka Asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (Akuvikiru), Simon Ndallu, aliiomba jamii kushirikiana na serikali ili kuhakikisha wanafunzi wote wa kidato cha kwanza wanaanza masomo

**Abdul Mitumba, Ruangwa na Waandishi Wetu Mbulu, Katavi**

KATIKA jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kila mtoto anapata elimu, watendaji wameanza kulivalia 'njuga' suala hili ili kila mwanafunzi apate haki yake ya msingi ya elimu.

Rais Dk. Samia amejenga shule na madarasa mengi katika kila halmashauri nchini kuanzia shule za awali, msingi na sekondari kupitia miradi ya Scoop na Sequip.

**Ruangwa**

Kwa kuitikia wito huo wa Rais, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Hassan Ngoma, alifanya ziara ya kushtukiza katika shule mbili za sekondari za Kata ya Mandawa na Chunyu.

Katika ziara yake, Ngoma alibaini kuwa jumla ya wanafunzi 40 wa kidato cha kwanza kati ya 247 waliopaswa kuripoti kuanza masomo Januari 8, mwaka huu, ndiyo walioripoti katika shule hizo kati ya shule 26 zilizopo wilayani hapa.

Wanafunzi 30 kati ya 133, wameripoti Shule ya Sekondari ya Kata ya Mandawa na wanafunzi 10 kati ya 114 wameripoti na kuanza masomo katika Sekondari ya Kata ya Chunyu.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Wilaya Ngoma aliwaagiza maafisa elimu kata husika na nyingine zote za wilayani humu, kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kuanza masomo, wanaanza kwa wakati.

Alitoa agizo hilo katika wiki ya kwanza ya shule kufunguliwa baada ya kufanya ziara ya kufuatilia zoezi la wanafunzi kuanza masomo katika Sekomdari za Chunyu na Mandawa ndipo alipokutana na mahudhurio duni kiasi hicho.

Ngoma alilazimika kuingia madarasani ili kujiridhisha idadi hiyo ndogo ya wanafunzi, hali ambayo ilionekana dhahiri kumsononesha.

"Maafisa elimu, naomba mfanye ufutiliaji wa karibu na haraka ili wanafunzi wote ambao bado hawajaripoti, wafanye hivyo kwa wakati," alisema.

Katika ziara hiyo, DC Ngoma aliambatana na Maafisa Elimu Msingi na Sekondari, ambapo pia alitoa wito kwa wazazi na walezi kuweka mkazo kuhakikisha watoto wanawapeleka shule haraka.

Akizungumzia hali hiyo na agizo la DC Ngoma, Ofisa Miradi kutoka Asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (Akuvikiru), Simon Ndallu, aliiomba jamii kushirikiana na serikali ili kuhakikisha wanafunzi wote wa kidato cha kwanza wanaanza masomo.

Ndallu ambaye shirika lake limekuwa likiratibu na kutekeleza miradi ya elimu kwa muda mrefu wilayani humo, alisema siyo sahihi jukumu hilo kuwaachia maafisa wa serikali na wazazi pekee.

**Katavi**

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Onesmo Buswelu, amesema hajaridhishwa na kasi ya wanafunzi waliofaulu kwenda kidato cha kwanza kuripoti shuleni.

Alisema hayo baada ya kukagua wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Kabungu huku akiahidi kupita kila kona ikiwemo nyumba kwa nyumba kuwasaka wanafunzi hao.

Alitoa ahadi hiyo wakati akizungumza na wanafunzi katika shule hiyo jana ambapo alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri na timu yake, kutumia jeshi la akiba kuwatafuta wanafunzi ambao bado hawajaripoti shuleni.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kabungu, Abdallah Kombo, alisema wamepangiwa wanafunzi 231 na mpaka sasa ni wanafunzi 30 ambao wameripoti.

Aidha, Buswelu alisema hakuna mwanafunzi yeyote anayetakiwa kuripoti akiwa na dawati pamoja na mifuko mitano ya saruji kama inavyodaiwa.

**Mbulu**

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Kheri James, naye kwa upande wake alifanya ziara ya kikazi katika shule za msingi na sekondari za halmashauri mbili wilayani humo kufuatilia zoezi la kupokea wanafunzi pamoja na mwenendo wa masomo.

Akizungumza katika ziara hiyo, James aliwapongeza wakurugenzi na wakuu wa shule kwa kusimamia vyema zoezi la kupokea wanafunzi na kuwataka kuhakikisha ratiba za masomo zinaendelea kwa wanafunzi ambao tayari wamewasili shuleni.

Alitumia fursa hiyo kuwaeleza wakuu wa shule katazo la serikali la kuwarudisha nyumbani watoto kwa sababu ya michango au masharti mengine yoyote ambayo yanapingana na miongozi ya elimu.

Aidha, aliwahimiza wazazi, viongozi na wananchi kuhakikisha kuwa kila mtoto anayestahili kuwa shule anafikishwa shuleni.

**Njombe**

Wanafunzi 12,000 kati ya 21,356 waliofaulu na kupangiwa kuanza kidato cha kwanza katika shule mbalimbali mkoani Njombe, sawa na asilimia 43.9 hawajaripoti shule.

Ofisa Elimu wa mkoa huo, Mwalimu Nelasi Mulungu, alisema hayo wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa kutembelea shule mbalimbali kukagua hali ya wanafunzi kuripoti shule.

Baada ya kutembelea Shule za Sekondari Lunyanywi na Mpechi mjini Njombe, Mulungu alisema hadi Januari 15, mwaka huu, wanafunzi 9,356 pekee ndiyo walioripoti shuleni.

Alisema hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa dhidi ya watoto ambao hawajaripoti.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mpechi, Brown Kiswaga, ambaye alisema shule hiyo kwa sasa haina changamoto yoyote hivyo anawaomba wazazi kuwapeleka shule watoto waliopangiwa hapo.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kuruthum Sadick, alisema hakuna mtoto atakayeachwa nyumbani ilhali amefaulu wazazi wao watachukuliwa hatua za kisheria.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema hakuna sababu ya mzazi kutompeleka shule mtoto wakati waliondoa vikwazo vingi.

Nao baadhi ya wazazi ambao wameshawapeleka watoto shule, waliitaka jamii kutambua umuhimu wa elimu huku baadhi ya wanafunzi nao wakiwaasa wanafunzi wenzao kuzingatia masomo.

# Shanga yatolewa kwenye mapafu ya mtoto MNH

**Na Mwandishi Wetu**

JOPO la Madaktari Bingwa wa Upasuaji wa kifua, moyo, mapafu na mfumo wa upumuaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), wamefanikiwa kuondoa shanga ya plastiki iliyokuwa imekwama katika pafu la upande wa kulia la mtoto mwenye umri wa miaka mitano.

Daktari Bingwa wa Mapafu na Mfumo wa Upumuaji wa MNH, Dk. Mwanaada Kilima, alisema shanga hiyo iliingia kwenye pafu baada ya kumpalia mtoto alipokuwa akiichezea mdomoni takribani mwezi mmoja uliopita.

Dk. Kilima alifafanua kuwa mtoto huyo alitaabika tangu wakati huo kwa kikohozi na kupumua kwa shida, huku njia mbalimbali zikitumika kujaribu kuitoa bila mafanikio na ndipo wataalamu wa mapafu walipofanikiwa kuitoa bila madhara yoyote.

"Tulitumia mpira laini wenye kamera ya video ya mapafu (Flexible Bronchoscope) na kifaa cha kukamatia (foreign body basket) na kufanikiwa kuitoa, hivyo kumwepusha mtoto huyo na upasuaji mkubwa ambao ungesababisha ama kutoa pafu au sehemu ya pafu," alisema Dk. Kilima.

Kwa upande wake, Dk. Ramadhan Hamis, Bingwa wa Upasuaji wa kifua na moyo, ndiye aliyeongoza jopo hilo kwa kushirikiana na Dk. Charles Komba ambaye ni Bingwa wa Upasuaji kifua pamoja na Dk. Kilima, Bingwa wa mapafu na mfumo wa upumuaji.

Kwa msingi huo, madaktari bingwa hao, wameshauri wazazi kufuatilia michezo ya watoto kwa karibu zaidi na kuwazuia kuweka vitu mdomoni, puani na maskioni ili kuwaepusha na madhara mbalimbali yakiwemo ya kudumu na kifo.





# Konokono wazua sintofahamu mashamba ya kahawa Mbozi

**Na Lauden Mwambona, Songwe**

VIUMBE aina ya konokono wenye vibuyu mgongoni, wamevamia zao la kahawa na kushambulia majani na punje kwenye miti katika Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, hali inayouza hofu kwa wakulima.

Wakulima wa kahawa , Lais Mkoma wa Kijiji cha Iwalanje Kata ya Magamba, Fikiri Sampamba wa Kata ya Hasanga na Lamson Mgalla wa Kata ya Isansa, kwa nyakati tofauti walisema konokono wamekuwa kero kubwa kwa zao la kahawa.

Walisema wamejaribu kuwaua kwa aina mbalimbali za viuatilifu, lakini bila mafanikio.

Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, George Nipwapwacha, alithibitisha kuwepo kwa wadudu hao tangu mwaka 2022.

Nipwapwacha alisema kwa mara ya kwanza wakulima waliripoti tatizo la kuwepo kwa konokono maeneo ya Old Vwawa na kwamba serikali inaendelea kufuatilia suala hilo.

"Taarifa za konokono zimefikishwa Wizarani," alisema.

Aliongeza kuwa walianza kutoa ushauri wa kuwakusanya konokono na kuwaua, lakini sasa wanawashauri wakulima kutumia dawa aina ya ' konokono bite.'

Kwa upande wake, Meneja wa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TACRI) iliyopo Mbimba mjini Vwawa, Dismass Pancras, alipoulizwa kuhusiana na kero hiyo, alisema taasisi ilipata changamoto hiyo miaka mitatu iliyopita.

Pancras alisema maeneo yaliyoripotiwa ni mengi yakiwamo za Kata za Nyimbili, Igamba na Isansa.

Alisema TACRI Mbimba wanaendelea na utafiti baada ya ushauri wa kuwaokota na kuwamwagia chumvi kushindikana.

Alisema kwa sasa wakulima wa kahawa wanashauriwa kuwaua kwa kutumia dawa ya konokono bite.

Wakizungumzia sababu za konokono hao kuanza kula kahawa, Meneja Pancras alisema wanaamini ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi ndiyo chanzo.

Alisema upo uwezekano kwa sasa wanazaliana kwa wingi kuliko zamani.

Naye Nipwapwacha alisema upo uwezekano ndege waliokuwa wanakula konokono, lakini kwa sasa hawapo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mtandao, konokono wenye vijumba pamoja na upole wake, hula aina 500 tofauti za mimea.

Kamishna wa Kilimo huko Florida nchini Marekani, alisema konokono hao ni tishio pia kwa afya ya binadamu.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Kamateni hawa watu



Huku mitaani kwenye vichochoro vyetu kuna tatizo la watu kutiririsha majitaka hasa pale mvua inaponyesha.

Mbaya zaidi, maji wanayotiririsha yanatoka vyooni au kwenye makaro ya maji taka. Hii ni mbaya sana hasa kwa kuzingatia kuna kipindupindu. Mabwana afya kamateni hawa watu.




MAONI YA MHARIRI

# Mzazi asiyezingatia elimu asiachwe

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imejenga madarasa kuhakikisha watoto waliofaulu kuingia kidato cha kwanza wanaingia darasani.

Pesa hizo zingeweza kufanya shughuli nyingine kama kujenga barabara, kuongeza mishahara ya watumishi wa sekta ya umma na mengine lukuki lakini kwa kutambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa Tanzania, mabilioni ya fedha yanapelekwa huko.

Ni katika muktadha huohuo, serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 18 kila mwezi ili kugharimia elimu bila ada.

Serikali iliamua kujitwisha mzigo huo ili kumpunguzia mzazi uzito wa kusomesha kwa kufuta ada na michango mbalimbali.

Kwa nini serikali inafanya yote haya? Ni kwa sababu inajua umuhimu wa elimu kwa watoto wa Tanzania. Nchi yetu inataka wananchi walio elimika kuanzia mama wa nyumbani, mkulima hadi ofisa mwandamizi serikalini. Inataka wataalamu mbalimbali. Huwezi kuwapata bila kupitia mfumo wa elimu.

Serikali inatambua kwamba taifa la watu mbumbumbu haliwezi kusonga mbele kwa haraka. Ukiwa na wakulima mbumbumbu, kwa mfano, ni vigumu kuwapa elimu kuhusu kilimo cha kisasa wakaelewa haraka.

Serikali inajua elimu ni ufunguo wa maisha na inasemwa kwamba namna nzuri na sahihi ya kumsaidia mtoto wa maskini ni kumpa elimu.

Wakati shule zikiwa zimefunguliwa tangu tarehe 8 mwezi huu, idadi ya wanafunzi walioripoti kuanza kidato cha kwanza katika baadhi ya shule nchini ni ya kusikitisha.

Kwa mfano, takwimu zinaonesha kwamba katika mkoa wa Njombe hadi jana walikuwa wameripoti wanafunzi 9,356 tu kuanza kidato cha kwanza kati ya 21,356 waliotakiwa wawe wameripoti.

Wanafunzi walioripoti katika Shule ya Sekondari ya Chunyu iliyoko Ruangwa hadi jana walikuwa 10 tu kati ya 114 wanaotakiwa kuripoti.

Sababu kubwa ambayo imekuwa ikitajwa kuwafanya wazazi kutohakikisha watoto wao wanaendelea na masomo ni kutoona umuhimu wa elimu.

Wapo wazazi wanaotaka watoto wao wa kike waolewe, wengine wanataka wafanye kazi za ajira zikiwemo za kilimo, ufugaji, kwenye migodi na majumbani na wengine wanataka wawatumikishe watoto wao kwenye biashara. Kimsingi hawa ni watu wasiojali mustakabali wa baadaye wa watoto wao.

Katika hali hii, serikali isikae kimya. Lazima wazazi wa aina hii walazimishwe na vyombo vya dola kuwapeleka watoto shule kupata elimu kwa faida ya watoto hao na Taifa kwa ujumla.

Katika gazeti hili tuna taarifa ya Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Hassan Ngoma, kufanya ziara ya kushtukiza katika shule mbili za sekondari za Kata ya Mandawa na Chunyu na kujionea namna wazazi wasiojitambua walivyoshindwa kuwaandikisha watoto wao kuanza kidato cha kwanza.

Ni vyema, kama alivyoagiza Ngoma, maofisa elimu wa kila kata nchini kote wakahakikishe wanafunzi wote waliochaguliwa kuanza masomo, wanaanza.

Jamii nzima pia ishirikiane na serikali kuwafichua, kuwapa elimu na kuwasema wazazi wasiojitambua kuhakikisha watoto wao wanakwenda shule.

Kwa kutumia mgambo na askari polisi, wazazi wanaokwamisha watoto wao kupata elimu, tena bila malipo, wasiachwe hivihivi. Watiwe msukosuko na kuhakikisha watoto wanasoma. Elimu ni haki yao ya msingi.

## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com

JICHO LANGU

Na Abdul Mitumba, Ruangwa

# Wanahabari zingatieni haya -2

MWAKA huu wa 2024, Tanzania inatarajiwa kuwa na uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, kabla ya Uchaguzi Mkuu wa rais, wabunge na madiwani mwakani.

Ni kipindi adhimu kwani ndicho kitakachotupa wawakilishi wetu wa kisiasa katika kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Moja ya wadau muhimu katika kuwafikishi wananchi habari, ni waandishi wa habri.

Kwa kujua umuhimu wao, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), umeviomba vyombo vya habari vya ndani kujiandaa kikamilifu ili kuripoti kwa haki matukio yanayohusu haki za wanawake katika kugombea, kuchagua na kuchaguliwa nafasi mbalimbali za uongozi katika changuzi mbili kubwa zijazo.

> **Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), umeviomba vyombo vya habari vya ndani kujiandaa kikamilifu ili kuripoti kwa haki matukio yanayohusu haki za wanawake katika kugombea, kuchagua na kuchaguliwa...**

Wakati wote wa uchaguzi, vyombo vya habari ni mhimili mkuu unaounganisha wagombea na wapiga kura, pamoja na kutoa viashiria vinavyoweza kusababisha vurugu na machafuko," imesema sehemu muhimu ya Ilani hiyo TGNP na washirika wake yenye kusara 39.

Ilani inasema ni vyombo vya habari vyenye uwezo wa kutoa fursa na jukwaa la kujadili masuala vyeti yanayohusu mustakabali wa taifa kwenye maeneo mengi ikiwemo ya jinsia.

Pia TGNP na washirika wake wanasema vyombo vya habari vina nguvu kubwa ya kuwezesha mabadiliko ya mfumo kandamizi kwa kukemea ubaguzi wa aina yoyote, vitendo vya rushwa hasa ya ngono kwa wagombea wanawake wakati wa uchaguzi.

TGNP imeainisha maeneo 13 yanayopaswa kuzingatiwa na vyombo vya habari wakati wa uchaguzi, kuanzia kuandikisha wapiga kura, wagombea kuchukua fomu, kurudisha, kampeni na kutangazwa matokeo.

Katika toleo liliopita, tuliangalia maeneo matano muhimu. Leo tunaangalia yaliyobaki:

Sita, TGNP inasema, ni vizuri uwepo uhakiki wa kweli wa habari zinazoandaliwa na kuwasilishwa katika vyumba vya habari zinazohusu haki za wanawake na kuzipa kipaumbele hasa zile zenye ujumbe chanya unaokemea jumbe hasi.

Saba, waandishi wa habari watoe taswira chanya kwa wanawake wanaowania nafasi mbalimbali za kuchaguliwa.

Nane, kuhakiki matumizi ya lugha ili kuondoa zile zenye ukakasi zinazodhalilisha wanawake, hasa wagombea.

Tisa, kuwapa wanawake wagombea nafasi ya kwanza kwenye kurasa za habari au vichwa vya habari.

10, wanahabari wanapaswa kujielimisha kuhusu masuala ya jinsia katika mchakato wote wa uchaguzi ili kubaini mapengo ya utekelezwaji wa sheria za uchaguzi kwa mrengo wa jinsia.

Maarifa haya yatawapa wanahabari nyenzo ya kutetea haki ya ushiriki wa wanawake katika mchakato wa uchaguzi.

11, vyombo vya habari viunganishe nguvu na watetezi wa haki za wananchi hususan za wanawake katika kutetea haki zao za ushiriki kwa kutumia vyombo husika.

12, wadau mbalimbali waunganishe nguvu ili kuwawezesha wagombea wanawake hususan vijana, kutumia vyombo vya habari katika kampeni zao.

Sehemu ya 13 ya Ilani hiyo, TGNP inasema Baraza la Habari (MCT) na wadau wengine wa habari waandike ripoti ya mchakato wote wa uchaguzi itakayolenga kueleza jinsi vyombo vya habari vilivyohusika na ama jitihada za kubomoa fikra za kumdhalilisha mwanamke au vilivyoweza kushiriki kwenye kubomoa mfumo wa kifikra kuhusu ushiriki wa wanawake katika zoezi lote la uchaguzi.

Katika Ilani hiyo, TGNP na washirika wake wameitaka Taasisi ya Kuzua na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), wakisema ni muhimu ikajipambanua kama chombo huru kinachofanya kazi zake kwa weledi, uwazi na haki ili kiendelee kuheshimika. (Tukipata nafasi pia tutaangazia eneo hili).ika jamii.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda.

# Tanga Mpo? Mjiandae, Makonda huyo Jan 20

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, anatarajiia kuanza ziara ya kikazi mkoani Tanga.

Ziara hiyo inatarajiwa kuanza Januari 20 hadi 22, mwaka huu.

Akizungumza ofisini kwake, Katibu wa CCM Mkoa wa Tanga, Selemani Sankwa, alisema ziara hiyo ni ya kikazi ambayo itaambatana na kufanya mikutano ya hadhara katika wilaya za Pangani, Tanga, Muheza na Korogwe.

"Ziara hii tunategemea itaendelea kutuimarisha kama Chama kwa kutatua changamoto na kusukuma miradi ya kimkakati inayotekelezwa mkoani Tanga ili ikamilike kwa wakati. Hii itasaidia kufikia lengo letu la kushinda mitaa yote 263, vijiji vyote 775 na vitongoji vyote 4,572 vya Mkoa wa Tanga kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba, mwaka huu," alisema Sankwa.

> **Ziara hii tunategemea itaendelea kutuimarisha kama Chama kwa kutatua changamoto na kusukuma miradi.**

# Makosa ya uhalifu Arusha yapungua

**Na Mwandishi wa Jeshi la Polisi, Arusha**

MAKOSA mbalimbali ya uhalifu mkoani Arusha, yamepungua ikilinganishwa na mwaka 2022.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, ACP Justine Masejo, kwa mwaka 2022, makosa ya uhalifu yalikuwa 2,995 na mwaka jana (2023), yalipungua na kufikia 2,634 ikiwa ni pungufu ya makosa 361.

Kamanda Masejo alifafanua kuwa kiwango hicho cha kupungua kwa makosa ni sawa na asilimia 12.

Aidha, alisema jumla ya watu 533 walihukumiwa kifungo jela baada ya kupatikana na makosa mbalimbali yakiwemo ya ubakaji na ulawiti mkoani humo katika kipindi cha mwaka jana.

Kamanda Masejo alifafanua kuwa jumla ya watuhumiwa 138 wa makosa ya ubakaji, walihukumiwa vifungo mbalimbali gerezani, 86 vifungo vya maisha jela, 37 jela miaka 30 jela na wengine 15 jela miaka 20.

Upande wa makosa ya ulawiti, alisema jumla ya watuhumiwa 103 walihukumiwa vifungo mbalimbali jela, 89 kifungo cha maisha na 14 jela miaka 30.



Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, ACP Justine Masejo.



Mkuu wa CBE, Profesa Edda Lwoga.

# CBE yaanza kuwanoa wahudumu wa mabasi

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeanza kutoa mafunzo kwa wahudumu wa kwenye mabasi ya abiria ili kuifanya kazi hiyo kuheshimika kama zilivyo fani nyingine.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa CBE, Profesa Edda Lwoga, wakati wa uzinduzi wa mafunzo hayo.

Profesa Lwoga alisema katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, CBE imeamua kutoa mchango wake katika kukuza weledi na ufanisi wa wahudumu wa usafiri wa umma.

Alisema lengo ni kuhakikisha huduma hizo zinakuwa na ubora wa hali ya juu na kwamba CBE ni miongoni mwa taasisi ambazo zimepewa kibali cha kutoa mafunzo hayo.

Profesa Lwoga aliongeza kuwa tayari chuo kimeshaandaa mitaala, mwongozo wa mafunzo pamoja na kuandaa wawezeshaji na vitendea kazi vyote muhimu kwa mafunzo hayo.

"Ni matarajio yetu kuwa mara tu baada ya uzinduzi huu, chuo kitaanza rasmi udahili wa washiriki wa mafunzo na yatafanyika katika vituo vilivyoko katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya," alisema.

"CBE inatambua juhudi zilizofanywa na serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra), katika kuboresha usafiri wa barabara nchini," alisema.

Alifafanua kuwa kuanzishwa kwa Latra kupitia Sheria ya Udhibiti wa Usafiri ya mwaka 2019, ilikuwa hatua muhimu katika kusimamia na kuboresha sekta hiyo muhimu.

"Hata hivyo, bado tunashuhudia sekta hii ikiendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uvunjifu wa sheria na kanuni za usalama barabarani, huduma kwa wateja isiyoridhisha, hali hii inahitaji jitihada zaidi kutoka kwa wadau wote," alisema.

Mkuu wa Dawati la Elimu ya Usalama Barabarani wa Jeshi la Polisi, Michaek Deleli, alisema Jeshi hilo linaona mafunzo hayo ni fursa kubwa kwa sababu yataondoa changamoto nyingi za barabarani kwenye usafiri wa umma.

"Kuna mambo yanafanyika ya kiuhalifu kwenye usafiri wa umma na yanatokana na wahudumu kutokuwa na elimu sahihi, mfano tumeshuhudia kusafirishwa kwa wahamiaji haramu vitendo vinavyofanywa na wahudumu wasio na mafunzo wala kujua sheria za nchi," alisema.

Alisema hata dawa za kulevya zinasafirishwa kupitia magari hasa mabasi, lakini yanapokamatwa wahudumu wanashindwa kuwatambua wamiliki hali ambayo imekuwa ikisababisha changamoto.

"Kwa mfano, tunapokamata mzigo haramu kwenye basi, utakuta mhudumu wa basi hajui ni wa nani na ukiwauliza hata abiria wanaukataa, lakini wakipata mafunzo haya wataweweka mizigo kwa namna ambayo kila mwenye mzigo atatambulika kwa urahisi," alisema.

Mweka Hazina wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (Taboa), Mbazi Mjema, aliipongeza serikali kwa uamuzi wa kuanzisha mafunzo hayo kwani yatasaidia chama hicho kutimiza majukumu yake na utendaji wa kazi utaboreshwa.

"Tuna wafanyakazi wengi wa darasa la saba, kwa hiyo vyeti watakavyopata ni mali yao wakihama kampuni moja kwenda nyingine, cheti kinabaki ni mali yao binafsi kwa hiyo tupunguzieni ada ya mafunzo ili tuwapeleke mafunzo wahudumu wengi," alisema.

# Silaha kali zinazotumiwa na Hamas kupigana na Israel

KUNDI la wanamgambo wa Hamas, linatumia silaha za hali ya juu katika vita vyake dhidi ya Israel, Uchunguzi wa kitaalamu wa BBC Arabic umegundua.

Wataalamu wa masuala ya kijeshi wanasema baadhi ya silaha zinazotumiwa zimefanyiwa marekebisho na kuwa hatari zaidi ikilinganishwa na mashambulizi ya awali.

Oktoba 7, mwaka jana, Hamas ilivuka Gaza na kuingia Israel katika shambulio ambalo halijawahi kushuhudiwa lililohusisha kurusha mamia ya roketi na makombora, kutumwa kwa ndege zisizo na rubani zenye vilipuzi na utumiaji wa idadi isiyojulikana ya silaha ndogo na risasi.

Iliua Waisraei 1,200 na kuwachukua mateka zaidi ya 240 kurudi Gaza. Tangu wakati huo, mashambulizi ya anga ya Israel na uvamizi wa ardhini huko Gaza, yamesababisha vifo vya zaidi ya Wapalestina 23,000.

BBC News Arabic imetambua silaha nne zinazotumiwa na Hamas na tawi lake la kijeshi, Brigedi ya al-Qassam, ambazo zimezua maswali kuhusu uwezo wake na jinsi inavyonunua sehemu za kuunda silaha hizo.

Jeshi la Israel (IDF) linasema kuwa limewaua wapiganaji 8,000 wa Hamas, idadi inayopingwa na kundi hilo, ambalo limetangazwa kuwa shirika la kigaidi na Uingereza na nchi nyingi za Magharibi. Israel inasema wanajeshi wake 187 wameuawa huko Gaza hadi kufikia sasa.





### Kombora la la 'Yasin 105'

Kombora la Yasin 105 mm la kuzuia vifaru, limeonekana kwenye video mbalimbali zilizoshirikiwa na al-Qassam Brigades tangu kuanza kwa mashambulizi ya ardhini ya Israel, ambapo linaonyeshwa likilenga vifaru vya Israel Merkava huko Gaza.

Kombora hilo limepewa jina la Sheikh Ahmed Yasin, marehemu mwanzilishi wa vuguvugu la Hamas na linarushwa kutoka RPG lililoundwa na Urusi.

Brigedia Jenerali wa zamani wa Jeshi la Misri, Samir Ragheb, anasema muundo wa vichwa viwili vya Yasin 105 ni uvumbuzi muhimu.

Chaji ya kwanza ya mlipuko inalenga silaha za kifaru, kuruhusu kuingia kwa sehemu au kamili, wakati chaji ya pili inahakikisha kupenya kamili ndani ya kifaru, kukilipua, anasema.

Philip Ingram, afisa wa zamani wa ujasusi wa eshi la Uingereza, anasema masafa madhubuti ya kombora hilo ni mita 150 - 500 na kasi ya juu ya mita 300 kwa sekunde.

Pia anasema usahihi unaohitajika kwa muundo huu wa vichwa viwili vya vita, unaonyesha uwezo wa juu wa kutengeneza silaha wa Hamas.

Vifaru vya Israel vina mfumo wa kuzuia makombora yanayopenyeza anaongeza.

Lakini kumekuwa na taarifa kwamba mfumo wa Israel umetatizika na kombora la Yasin. BBC News Arabic haijathibitisha hili.

Wataalamu wa kijeshi wanakadiria kuwa Hamas ina hifadhi kubwa ya angalau makombora 2,000 ya Yasin 105.



### Topido ya 'Al Asef'

Katika video iliyotolewa na Hamas mwishoni mwa Oktoba, mwaka jana, kundi hilo la wanamgambo lilionyesha silaha mpya, 'Al Asef' silaha , ambayo walisema waliitumia katika shambulio la Oktoba 7, mwaka jana.

BBC News Arabic imethibitisha kuwa video hii haikuwekwa mtandaoni hapo awali.

Wataalamu wanasema silaha hii ni gari lisilo na rubani au linaloendeshwa kwa mbali chini ya maji, iliyoundwa kwa ajili ya shughuli za chini ya maji.

### Kilipuzi cha 'Shawaz'

Silaha nyingine inayoonekana kwenye video za Hamas kwenye mitandao ya kijamii ni 'The Shawaz', neno la Kiarabu linalomaanisha moto, kilipuzi kilichotengenezwa na Hamas kinachotumiwa kuvizia magari kwa karibu.

Mrengo wa kijeshi wa Hamas umethibitisha kuwa ulizitumia wakati wa mashambulizi ya ardhini ya Israel huko Gaza.

Israel pia imeonyesha idadi kubwa ya silaha hizi kutoka Gaza ambayo inaonyesha juhudi kubwa za uzalishaji wa ndani.

Julai, mwaka jana, vikosi vya al-Qassam vilitoa video inayoonyesha vifaa hivi vya vilipuzi, ambavyo vimeunganishwa na waya.

Ingram anasema Hamas inatumia mfumo ulioboreshwa katika mzozo huu, ambao una uwezo wa kuharibu magari ya kivita ya Israel.

Anasema vifaa hivyo vinajumuisha diski ya chuma, ambayo kawaida hutengenezwa kwa shaba, iliyozama ndani ya vilipuzi.

Baada ya mlipuko, diski ya shaba inabadilika kuwa kifaa chenye makali, ikipenya silaha za magari yaliyolengwa.

Urahisi wa vifaa hivi kupatikana ni tofauti na muundo na matumizi yao tata.

Wakati sehemu yenye changamoto kubwa iko katika kupata na kuunda kwa usahihi diski ya shaba, Hamas imeonyesha uwezo wa kuzitengeneza, anaongeza.

Mashambulizi ya anga ya Israel huko Gaza yameharibu miundo mingi ambayo Hamas inaweza kutumia kurejesha vifaa vya ujenzi kwa ajili ya silaha

### Hamas wanaendeleaje kutengeneza na kupata silaha?

Hamas inayaunda upya mabomu ya Israel ambayo hayajalipuka pamoja na kutumia tena chuma na nyaya kutoka kwa majengo yaliyoharibiwa.

Brigedia Jenerali Ragheb, anasema Iran imesaidia kusafirisha silaha katika Ukanda wa Gaza, huku kukiwa na mahandaki ya siri kwenye mipaka ya Gaza na boti zikijaribu kupenya kwenye vizuizi vya Israel katika Bahari ya Mediterania.

Yasser Hashem, Mkuu wa zamani wa Jeshi la Misri, anapendekeza udhibiti wa Israel juu ya mipaka yake usiwe kamilifu, akiashiria kuwepo kwa safu ya kimataifa ya magendo ambayo inaingia Israel kutoka Lebanon.

Mamlaka ya Israel ilitangaza Septemba, 2022 kwamba ilizuia jaribio la kusafirisha vilipuzi kwenye kivuko cha Kerem Shalom kuelekea Gaza. Vilipuzi hivyo vilifichwa kwenye shehena ya nguo.

BBC.



Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

# JARIDA Jungu kuu

| Jumatano Januari 17 - 23, 2024 |




# Chadema wanaandamana kwa lipi?



UK. 12 & 13

Siasa



# Hivi mwana-CCM anayefikiria kumpinga Samia anataka nini?

**Na Hamid Yassin**

KUMEKUCHA! Kila kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) anataka Mwenyekiti, Dk. Samia Suluhu Hassan ndiye abebe dhamana ya kuwania urais kwenye uchaguzi mkuu wa mwakani 2025 kwa tiketi ya chama hicho tawala.

Walianza viongozi wa ngazi za chini wa chama hicho na Serikali, lakini hivi karibuni tumesikia kauli za Makamu Mwenyekiti wa CCM, Comredi Abdulrahman Kinana na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaliwa Kassimu Majaliwa nao wakipendekeza mwakani kuwe na fomu moja tu maalumu kwa Dk. Samia ya kuomba kugombea urais wa Tanzania kwa tiketi ya chama hicho.

Kwa nini fomu moja? Maana yake viongozi hawa waandamizi wa CCM na serikali wanajua wazi ndani ya CCM kuna wahafidhina wanaoweza kuibuka na kumpinga Dk. Samia, Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuwania muhula wa pili wa kuongoza taifa letu.

Achilia mbali ule utaratibu wa kawaida wa CCM wa kumpa awamu mbili kila anayekuwa Rais wa Tanzania kwa tiketi ya chama hicho, mimi najiuliza hivi kuna MwanaCCM yeyote anaweza kuthubutu kujitokeza hadharani kumpinga Rais Dk. Samia akijifanya hajui makubwa ambayo Rais ameitendea nchi katika kipindi kifupi?

Ukisikia wakubwa wanasisitiza suala la lazima fomu iwe moja basi wanahisi au hasa wamesikia kuna vichwa maji kwenye chama hicho wanatamani kupambana na Samia uchaguzi ujao. Ingawa katiba ya nchi na hata ya CCM zinaruhusu lakini kama kuna Mwana-CCM atajitokeza basi huo utakuwa ni uchuro mkubwa!

Najua huko nyuma walijitokeza Wana-CCM wachache kutaka kuwapinga baadhi ya marais waliokuwa wakijiandaa kug katika awamu zao za pili za kuwania urais wa Tanzania kwa tiketi ya chama hicho, lakini hawakufanikiwa kufika kokote.

Kuna mwamba mmoja, kada wa CCM, akiitwa Munasa Sabi, ambaye kwa sasa ni marehemu, kama kumbukumbu zangu ni sahihi alikuwa akijitokeza mara kwa mara kuwapinga wagombea wa CCM waliokuwa madarakani.

Hata kada mwingine, kabla ya kuhamia upinzani, John Shibuda, knaye wakati wa Rais Jakaya Kikwete alijaribu kutaka kupambana naye ingawa hakufika mbali.

Vivyo hivyo ikitokea kwa Dk. Samia, Wallahi itakuwa kituko kama si uchuro kabisa! Yaani haya mazuri yote anayoendelea kuyafanya hadi sasa katika kipindi hiki kifupi cha miaka inayokaribia mitatu yatakuwa hayaonekani kwa mwana-CCM huyo au atakuwa anatafuta 'kiki' kama wanavyosema vijana wa leo?

## WAHAFIDHINA NDANI YA CCM

Naamini Comredi Kinana na Waziri Mkuu Majaliwa wanajua uwezo mkubwa wa Mwenyekiti wao huyo lakini wanachofanya hivi sasa ni kutimiza wajibu wao kama viongozi waandamizi wa CCM na Serikali kuwatahadharisha wahafidhina ambao Dk. Samia mwenyewe amewahi kutamka kwamba wapo ndani ya chama hicho!

Suala hili la wapingaji wa Serikali au uendeshaji wake ndani ya CCM lipo na lilithibitishwa na mwenyewe Rais Dk. Samia pale alipohudhuria Kongamano la Baraza la Wanawake la Chadema (BAWACHA) Machi 8 mwaka jana na kutoa hotuba iliyowavutia watu wengi ndani na nje ya nchi.

Pamoja na kwamba kitendo kile cha Dk. Samia kuhudhuria mkutano wa kisiasa ulioandaliwa na chama kikuu cha upinzani ndani ya nchi yake ni cha kihistoria, si kwa Tanzania tu bali karibu bara zima la Afrika, lakini wapo Wana-CCM ambao hawakukubaliana nacho!

Hotuba yake ile ilikuwa na maneno mengi ya busara, lakini nakumbuka yale ya kuwaasa viongozi wa Chadema kujiepusha na wahafidhina.

"Nimekuja hapa lakini naelewa kuna baadhi ya Wanachadema hawakufurahishwa na jambo hili, wanasema kwa nini mumwita rais kwenye jukwaa hili, Mwenyekiti (Mbowe) sasa ujue hata huku kuna wahafidhina, wengine wanasema Mbowe amelishwa asali huku wao wanakimbilia nje ya nchi na kung'ang'ania huko; Kwa hiyo Mwenyekiti uelewe huku kuna wahafidhina na kule kwangu pia wapo," alisema Dk. Samia kwenye kongamano lile.

Pamoja na Dk. Samia kukiri kwamba ndani ya CCM kuna wahafidhina, sielewi ni kwa nini bado hii dhana ya watu kufikiria kumpinga Rais Dk. Samia ndani ya CCM imekuwa ikiibuliwa mara kwa mara. Nakumbuka iliibuka huko nyuma lakini ilizimwa ndani ya Mkutano Mkuu wa CCM kule Dodoma mwaka juzi.

Rais mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete ndiye aliyepigilia msumari wa moto baada ya kuwepo kwa uvumi wa kumpinga Dk. Samia akisema upuuzwe kwani hakuna mwenye kumzidi sifa ya kugombea urais mwaka 2025 ndani na nje ya CCM!

Alinena haya mbele ya viongozi wote wa ngazi ya juu toka Bara na Visiwani na wajumbe wote wa mkutano ule mkuu.

Sasa kama aliyekuwa kiongozi mkuu wa CCM na Serikali kwa miaka kumi anaamini hakuna mwenye sifa ya kuwa kiongozi wa taifa hili kwa sasa zaidi ya Dk. Samia, hao WanaCCM wengine wanaohisiwa kutaka kumpinga hapo mwakani jeuri hiyo wanaitoa wapi?

Dk. Samia anajinadi mwenyewe kwa haya anayoendelea kuyafanya tangu aapishwe kuwa Rais wa Taifa hili Machi 19, 2021 na kama kuna MwanaCCM yeyote yule ambaye hayaoni na kudhani yeye ndiye anayestahili zaidi basi huyo ni wa kuogopwa kama ukoma!

Sina haja ya kuyarudia yote hapa kwani mwezi uliopita niliandika makala ndefu iliyoelezea mambo yote ya maendeleo aliyoyafanya katika kipindi hiki kifupi alichoongoza taifa hili.

Kumekuwepo na maendeleo chanya katika kila sekta ikiwemo zile zilizoonekana kuwa zimeshindikana kama vile utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, (WCF) ambao kwa miaka mingi ulikuwa umezorota lakini kutokana na mabadiliko ya kisera ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wake Dk. Samia sasa mambo ni safi.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma wakati akizungumza kwenye kikao kazi cha Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) kilichofanyika wilayani Bagamoyo Mkoani Pwani, alisema katika kipindi hiki cha utawala wa Dk. Samia, tozo mbalimbali zimepungua sana.

"Wafanyabiashara kwa maana ya sekta binafsi walipaswa kuchangia asilimia 1 ya mshahara wa mfanyakazi kila mwezi na ilipunguzwa hadi kufikia asilimia 0.5, kwa wafanyabiashara hii ni nafuu kubwa katika muktadha wa utekelezaji wa kuweka mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara Tanzania kuwa mazuri," alifafanua.

Jambo lingine ni kupunguzwa kwa kiwango cha riba cha asilimia 10 hadi asilimia 2 kwa mwezi kwa wanaochelewesha kuwasilisha michango ya kila mwezi.

"Mzigo huu ulikuwa ni mkubwa sana na ulikuwa unatishia wale ambao walipaswa kujisajili kwenye Mfuko kuja kujisajili, kupunguzwa kwa riba hii kumewavutia wafanyabiashara na hivyo kuongeza idadi ya wanachama kujisajili na Mfuko," alisema Dk. Mduma na kuorodhesha mafanikio mengine lukuki yaliyopatikana katika urais wa Samia.

## USAFIRISHAJI NA UMEME

Wale waliokuwa wanapigia kelele mkataba wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA) na Kampuni ya DP World ya Dubai sasa wametahayari kutokana na kasi ya mabadiliko ya utendaji wenye tija na ufanisi mkubwa!

Huku kampuni hiyo kubwa ikiwa bado inaendelea kusimika mitambo mikubwa ya kisasa, tayari ule mrundikano wa meli na foleni ya kusubiri kutia nanga bandarini unapungua kwa kasi sambamba na upakuaji wa mizigo ya ndani na ile inayopita kwenda nchi jirani.

Kwa upande wa ujenzi wa reli ya mwendo kasi Rais Dk. Samia ameagiza hadi kufikia mwezi Machi usafiri kati ya Dar es Salaam na Dodoma uwe umeanza ambapo hivi karibuni usafiri kati ya Dar na Morogoro utaanza rasmi.

Kwa upande wa mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP) ambalo wengi walidhani ujenzi wake ungesimama baada ya kifo cha mtangulizi wake, Rais John Magufuli, lakini jana uongozi wa Rais Samia umefanikisha kuwasha mitambo ya kuzalisha umeme kutokea kwenye bwawa hilo

Hatua hii inakwenda kuihakikishia nchi yetu umeme wa uhakika.

*Kwa mawasiliano na mwandishi wa makala haya; 0784 122020/ 0768 888787*



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457



# Tuzingatie tafiti hizi watoto kuangalia TV

SIKU moja, miaka takribani 10 nilikuwa nimeketi kwenye duka moja la vifaa vya maofisini (stationery) maeneo ya Mwembeyanga, Temeke, Dar es Salaam akaja dada mmoja akiwa na DVD takribani nne akitaka arudufishiwe pale dukani.

Nilishawishika kujua DVD zile ni za nini, mwanzoni nikidhani ni mmoja wa maharamia wa kazi za wasanii wetu ambao wakati walikuwa wakirudufisha kazi zao kinyemela, hali ambayo ilikuwa inawakosesha mapato wasanii wetu, wawe wa muziki ama wa filamu.

Ninakumbuka nilipoziangalia vyema samabamba na kumhoji, nikagundua kwamba zilikuwa ni DVD ambazo zimetengenezwa nje ya nchi kwa aili ya watoto na takriban zote zikiwa za vikatuni.

Katika maongezi yetu na dada huyo mrefu aliyenambia ana watoto watatu anaoishi nao, mmoja akiwa wa mdogo wake, alisema ameamua kuomba DVD hizo kwa jirani ili watoto wake wawe wakiangalia.

"Unajua nimegundua watoto wangu wanapenda sana TV, lakini wanaangalia mambo mengi ya hovyo. Hata hii mikanda ya filamu za Kitanzania nimegundua mingi si mizuri kwa watoto na ndio maana nimeazima hii ya vikatuni kwa jirani yangu nirudufishe ili wawe wanapata kitu cha kutazama," alisema.

Mimi nikamuuliza maswali matatu. La kwaza nilitaka kujua kama amewawekea watoto wake muda maalumu wa kuangalia televisheni ama ni pale wanapojisikia na pia kama kuna tabia yoyote tofauti ameiona kwa watoto wake anayohisi inatokana na kuangalia TV hadi kuamua kuchukua DVD hizo za vikatuni. Pia nilimuuliza kwa nini ana hizo za vikatuni pekee na si za masomo au mafundisho ya dini angalau hata moja kwa sababu pia zipo.

Yeye akajibu kwamba hajawawekea wanawe muda maalumu wa kuangalia TV na kwamba mara nyingi wakitoka shuleni wanafikia kwenye TV kama si kwenye chakula!

Kwa maelezo yake watoto wake, kama si chakula ama mazozi ya shule (homework) wanaweza kukaa wakiangalia TV hadi muda wa kulala!

Akasema ameamua kuanza na hizo za vikatuni alizomwazima jirani yake lakini atakwenda madukani Kariakoo kununua za masomo kama atafanikiwa kupata.

Kuhusu tabia, alisema wanawe wadogo, mkubwa akiwa darasa la tano. wamekuwa na tabia ya kuiga mambo mengi kwenye TV ikiwa ni pamoja na kupigana mateke, kupigana busu na kubwa zaidi ni kupenda kuimba nyimbo za Bongoflava ambazo wamezikariri kuliko masomo!

"Kwa mfano, mwanangu mkubwa wa kiume ambaye yuko darasa la tano nimegundua anapenda sana kumuiga mwanamuziki aitwaye Diamond kwa kuimba na hata vitendo vyake halafu mdogo wake anapenda ugomvi na kutishia wenzake bunduki," alisema.

Kadhalika alisema tatizo lingine la nyumbani kwake ni hausigeli wake. ambaye naye anapenda sana TV na hasa yeye na mumewe wanapokuwa kwenye mahangaiko yao kiasi kwamba siku nyingine anaunguza chakula.

"Huyu hausigeli wangu ni mzuri lakini anapenda sana TV na wakati mwingine anaunguza chakula kwa sababu ya TV. Ndiye pia amechangia watoto kupenda kuangalia mambo yanayowafaa wakubwa. Nimemuonya sasa awe akiwawekea watoto hizi katuni," akamaka dada yule.

Katika maongezi yetu nilimdokeza dada huyo ambaye ni jirani yangu umuhimu wa kuwapangia muda watoto kuangalia televisheni na kumweleza kwamba nilisoma mahala nikaona wakawa wanaeleza madhara ya kuruhusu watoto kuangalia TV kila wanapojisikia na kumwahidi kwamba nitapaangalia tena kisha nitaandika kwenye kona hii asome.

Kwa faida yake na wasomaji wangu, mahala nilikosoma taarifa zinazotokana na tafiti za mwaka 2007 zilizofanywa Marekani na taasisi ya American Academy of Pediatrics panasema hivi (kwa tafsiri yangu kutoka Kingereza kwenda Kiswahili ambayo si rasmi):

"Tabia ya watoto kuangalia televisheni kila siku kwa saa mbili ama zaidi huweza kusababisha watoto kukosa stadi za maisha zinazotakuwa katika jamii husika (poor social skills).

Kwa mujibu wa tafiti hizo, inapendekezwa kwamba watoto wenye umri chini ya umri wa miaka miwili wasiangalie kabisa TV na wale wenye umri zaidi ya miaka hiyo miwili wasiangalie zaidi ya saa mbili kwa siku.

Kisha wanaandika: "Tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba kuna athari kubwa kwa watoto wanapoachiwa kuangalia televisheni kwa muda mrefu. Kupunguza muda wa kuangalia sambamba na kuwachagulia vipindi ama vitu vya kuangalia kunapunguza athari ambazo watoto hawa ambao akili yao inapenda kunasa kila kitu kama kaseti mpya, wanaweza kuzipata."

Utafiti pia ulionesha kwamba kuwawekea watoto wa kuanzia miaka mitano na nusu televisheni kwenye chumba chao pia kuna matatizo ya kitabia ambayo watoto wanaweza kupata ikiwa ni pamoja na kuchelewa kulala na hivyo kusinzia madarasani.

Tafiti pia zinaonesha kwamba kuwaonesha watoto filamu zenye magomvi ama maneno machafu, huwafanya taratibu taratibu waone mambo hayo kama ya kawaida.

Nimalize kwa kuweka angalizo kwa wazazi wenzangu kuwawekea watoto muda maaluma wa kuangalia televisheni wasizidi saa mbili kwa siku ili wasiige mambo mengine yasiyofaa.

Imekuwa pia ikidaiwa kwamba baadhi ya hizi katuni zimekuwa zikifundisha watoto mapenzi ya kishoga kwa hiyo nazo ni za kuangalia sana.

Cha msingi pia ni kuchagua vipindi ama kuwawekea vitu vya kutazama na si kila kitu.

Kadhalika tuwe makini na wasichana wa kazi pale tunapokuwa hatupo majumbani kwa sababu nao wana mchango wao katika kuweka vipindi ama mikanda ambayo haina mafundisho mazuri kwa watoto.

Mtunzi mmoja wa mashairi aliwahi kuandika shairi akisema 'Sinema si neema' akimaanisha baadhi ya sinema hazifai kutazama.

**Tabia ya watoto kuangalia televisheni kila siku kwa saa mbili ama zaidi huweza kusababisha watoto kukosa stadi za maisha zinazotakuwa katika jamii husik**

Siasa



# Chadema wanaandamana kwa lipi?

**Na Hamid Yassin**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe ametangaza kuwa, kuanzia Jumatano ijayo (Januari 24 mwaka huu) watafanya maandamano ya 'amani' ya kupinga Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi.

Chadema inaitaka Serikali kuuondoa muswada huo bungeni eti kwa sababu hawajaridhishwa na mchakato uliofanywa wa ukusanyaji maoni, hivyo wataandamana nchi nzima kushinikiza azma yao hiyo itimie.

Kiongozi huyo wa Chadema anadai licha ya kuwepo kwa maridhiano ya kidemokrasia kupitia Sera ya Maridhiano ya Kidemokrasia ya Rais Samia Suluhu Hassan lakini anadai inataka kukwamishwa!

Kauli hii ya Mbowe inakuja wakati Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ikikamilisha sheria iliyosomwa bungeni Novemba 10, 2023 jijini Dodoma.

Miswada iliyosomwa kwa mara ya kwanza ni pamoja na ule wa Sheria ya Uchaguzi ya Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Mbowe anasema kwamba, katika kikao cha dharura walichokaa Kamati yao Kuu Januari 8 wiki iliyopita, chama hicho hakijaridhishwa na miswada yote hiyo na wanataka iondolewe Bungeni.

Anasema kwa muda mrefu yeye binafsi amepigania maridhiano na CCM huku akipingwa na viongozi na wanachama wenzake wa Chadema, lakini sasa anaungana nao kwani miswada hiyo imeonesha kutozingatia maridhiano hayo!

"Naagiza viongozi wa chama wa mikoa yote kuanza maandalizi ya maandamano, tunataka Serikali ujue hatuna utani. Viongozi wa mikoa, wilaya, kata na mitaa waanze maandalizi ngazi zote. Tutaratibu hadi kwenye sekretarieti tuhamasishe majirani kujitokeza. Itakuwa ni ruti yenye maumivu," anatishia Mbowe.

### NAFASI YA MJADALA IPO

Akijibu tuhuma hizo za Mbowe, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi amebainishwa kuwa, miswada hiyo ilipelekwa bungeni kwa utaratibu wa kawaida ndio maana wadau wakaruhusiwa kutoa maoni kwa lengo la kuboresha mahali watapoona kuna upungufu.

"Serikali imepeleka miswada bungeni kwa utaratibu wa kawaida, siyo hati ya dharura ambayo isingetoa nafasi ya mjadala, lakini njia ya kawaida kuna nafasi ya mjadala. Ndiyo maana Januari 4, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kushirikiana na Baraza la Vyama vya Siasa walifanya mkutano mkuu maalumu wa kujadili miswada hiyo," amefafanua Matinyi.

Ameongeza kuwa, jambo la kufanya hivi sasa ni wananchi na wadau kutoa maoni na mapendekezo yatakayoboresha kilichopo kwenye miswada hiyo yenye lengo la kuimarisha na kudumisha demokrasia.

"Tutumie nafasi hii kutoa maoni yetu, kwa nini Serikali iondoe kitu walichokileta kujadiliwa kwa utaratibu wa kawaida na sio hati ya dharura?" Amehoji Matinyi na kuongeza.

"Mkutano wa Ofisi ya Msajili ulikuwa mzuri na kulikuwa na Sekretarieti ya kukusanya maoni, tutoe maoni ya kuboresha lakini kamwe siyo kuuondoa bungeni au kufanya tukio lolote lisilotarajiwa," Matinyi anasisitiza.

### NJIA MBADALA IPO

Kwa lugha nyingine, Matinyi anashangaa kwamba ilichotakiwa kufanya Chadema ni kuitisha mikutano ya ndani ili kwanza kuwaambiwa wananchi kilichomo kwenye muswada huo na kutoa nafasi ya kutoa mapendekezo yao na kuyafikisha kwa wawakilishi wao walioko Bungeni. Hata kama kuna wabunge maalumu hawawatambui, lakini yuko mmoja wa kuchaguliwa ingawa mimi nimekuwa nikiona wabunge hao wasiotambuliwa na Chadema wamekuwa bado wakitetea maslahi ya upinzani.

Baada ya Rais Samia kuruhusu mikutano ya kisiasa ya hadhara ambayo ilifungwa na mtangulizi wake, Dk. John Magufuli Chadema wamenza tena mambo ambayo pengine wanaamini 'yanawaweka mjini' lakini ukweli ni kwamba ni kuleta vurugu tu katika nchi.

Nina hakika, kama maandamano hayo yataruhusiwa, asilimia 70 mpaka 90 ya waandamanaji (endapo watajitokeza) watakuwa hawajui chochote kuhusu kilichomo kwenye miswada huyo zaidi ya kufuata mkumbo tu!

Uzoefu unaonesha kila zinapokaribia nyakati hizi za kuelekea chaguzi za kitaifa mara nyingu ndipo chama hiki

kunapokurupuka toka kilipolala usingizi wa pono na kuanza kuzua taharuki miongoni mwa wananchi.

**CHADEMA HAWAJIAMINI?**

Niliwaona baadhi ya viongozi wa Chadema kwenye mkutano ule wa Msajili wa Vyama vya Siasa na Baraza la Vyama vya Siasa wakitoa michango yao ya wapi na kipi wanataka virekebishwe au Mbowe hawaamini wasaidizi wake?

Maana alikuwepo Katibu Mkuu wa Chama hicho, John Mnyika na Naibu Katibu Mkuu Bara, Benson Kigaila. Hawa wote walipewa nafasi ya kuchangia maoni yao; Je, Mbowe hawaamini viongozi wenzake hawa waandamizi? Mbona wao walimuamini kuhudhuria vikao vya maridhiano ya kisiasa na Rais Dk. Samia!

Tangu Mwenyekiti huyu wa Chadema aingie madarakani mwaka 2004, Chama hiki kinaonekana kuendeshwa kwa mihemko inayoitwa 'Maandamano na Oparesheni', tofauti na wakati kinaongozwa na akina Mzee Edwin Mtei na marehemu Bob Nyange Makani.

**WEKA HOJA MEZANI**

Mtindo huu wa uendeshaji chama kwa mihemuko badala ya kujenge hoja na kuweka mezani unaelezwa na baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa kwamba, hauna tija kisiasa kwa upande wa chama chao na kwa Taifa kwa ujumla wake.

Hoja yao kubwa ni kukosekana kwa agenda rasmi ambayo chama kinaweza kuisimamia katika harakati zake za kutafuta kuungwa mkono na wananchi.

Watanzania wa sasa wengi ni waelewa, ukiweka hoja mezani, kama ni ya msingi watakuelewa tu na kukuunga mkono na hata ndani ya CCM kuna wengi tu wanaoamini katika nguvu ya hoja na si hoja ya nguvu wanayotaka kuja nayo Chadema.

Aidha, wachambuzi hao wamekwenda mbele zaidi kwa kuufananisha mtindo wa chama kuendeshwa kwa mfumo huo kuwa sawa na chombo cha majini kuendeshwa na nahodha asiye na ujuzi.

Kwa mfano hakuna asiyejua kwamba Chadema huko nyuma walikuwa na ajenda ya ufisadi ambayo wenyewe walianza kuitangaza Kanda ya Ziwa walikokuwa wakiendesha kile walichokiita 'Operesheni Sangara'.

Kuanzishwa kwa operesheni ile mwaka 2007 kulikuja baada ya kushindwa kwa operesheni nyingine mbili walizozianzisha huko nyuma kwa mihemko na jaziba!

Kulikuwa na operesheni Chadema ni Tawi na Operesheni Chadema ni Msingi, zote hizo zilianzishwa kwa mbwembwe na majigambo kedekede.

Lakini si Watanzania wala Chadema wenyewe wanaoweza kusimama mbele ya kadamnasi wakajisifu na kudai kuwa, ziliwaletea manufaa, zaidi ya kukusanya makundi ya vijana mitaani na kuvuruga amani tuliyonayo.

Wachambuzi wengi wa masuala ya kisiasa wanakubaliana kuwa, lengo la wanaoanzisha siasa hizi za vuguvugu (Movement politics) ni kutaka jamii isiwasahau katika ulingo wa kisiasa, na si vinginevyo!

Na wanasema hali hiyo haitokei isipokuwa pale chama husika kinapokosa sera madhubuti inayoisimamia katika kuwashawishi wananchi wakiunge mkono.

Wakati wakizunguka mikoa mbalimbali hapa nchini kupaza sauti zao kuhusu orodha ya waliowaita mafisadi papa 11, akiwemo aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa ambaye baadaye walimchukua na kumfanya mgombea wao wa urais, walijiona wamepata ajenda ya kuwasaidia kuvuka katika uchaguzi Mkuu wa 2010.

Haukupita muda mrefu tukasikia kumeanzishwa Operesheni nyingine waliyoiita Movement For Change (M4C), ambayo kama zilivyo operesheni nyinginezo, haikuwa na manufaa yoyote. Kumbuka operesheni zote hizi zinaendeshwa kwa njia ya maandamano na mikutano ya hadhara!

Zitto Kabwe na wenzake waliondolewa Chadema baada ya kuandaa kilichoitwa 'Waraka wa Mabadiliko' ambamo, pamoja na mambo mengine walikuwa wanaona siasa za mihemuko na maandamano haziwezi kuwafikisha Ikulu!

Kabla sijaenda mbali, niseme kwamba sio lengo langu kutumia makala haya kuorodhesha Operesheni zote zilizowahi kutangazwa na Chadema kwa zaidi ya miaka 20 sasa tangu Mbowe awe Mwenyekiti wa Chama hicho mwaka 2004, hapana. Bali najiuliza peke yangu kwamba, ni mpaka lini vyama kama Chadema na washirika wake vitaacha lini siasa za ulaghai kwa Watanzania hasa vijana wetu kwa kisingizio cha Operesheni?

Julai 2016, Chadema ilizindua operesheni nyingine iliyopewa jina la Umoja wa Kupambana na Udikteta Tanzania (UKUTA). Ikaelezwa kuwa Operesheni ile ingekwenda sambamba na uzinduzi wa mikutano ya hadhara nchi nzima, ambayo ilipangwa kufanyika hadi Septemba Mosi, mwaka 2017.

Pamoja na mambo mengine, chama hicho kilidai lengo la operesheni ile ilikuwa kuzuia matukio ya ukandamizaji wa haki na demokrasia nchini, kiliyodai kuwa ilifanywa wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya urais wa hayati Dk. John Magufuli.

Binafsi nilijiuliza, hivi ni matukio yapi, iwe madogo au makubwa ya ukandamizaji haki yaliyofanywa na hayati Dk Magufuli mpaka kulihitajika kuanzishwa kwa Operesheni?

Kwa nini akina Mbowe na wenzake wanataka kutufanya Watanzania 'mazwazwa' na 'mazumbukuku'kwa kutumia operesheni na maandamano ili kutia doa amani yetu?

Ni kweli hayati Dk. Magufuli aliwazuia kufanya siasa za mitaani (za ndani ziliruhusiwa) kwenye nyakati ambazo si za chaguzi; Je, hivi sasa na Dk. Samia anafanya hivyo?

Ingawa mimi si msemaji wake, lakini Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama mnyenyekevu Dk. Samia Suluhu Hassan haijawahi kumzuia mtu au mwanasiasa kufanya siasa, ndiyo maana mpaka leo vyama vipo na hata viongozi wa vyama hicho zilizopo Buguruni, Dar es Salaam.

Operesheni ile iliyopewa jina la "Ondoa Msaliti Buguruni" (OMB) iliungwa mkono pia na baadhi ya wanachama wa CUF waliokuwa wanamuunga mkono aliyekuwa Katibu Mkuu wao, hayati Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Lipumba si mwenyekiti wao.

Wakati CUF ya Maalim Seif kwa usaidizi wa Chadema ilikuwa haitambui uenyekiti wa Lipumba, Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi kwa mujibu wa Katiba ya CUF yenyewe na sheria iliyounda vyama vingi, alimtambua Profesa Lipumba hadi hivi sasa.

Kwa mujibu wa aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Jacob Nkomola kutoka chama hicho na kwenda kuanzisha SAU iliyosajiliwa mwaka 2005, lakini CUF haikuwahi kuingilia kati.

Chadema haohao wameshakuwa na mzozo mkubwa kati ya Mwenyekiti wake wa Taifa na aliyekuwa Makamu wake, marehemu Chacha Wangwe, pia hatukusikia CUF wakiitisha waandishi wa habari na kutangaza kuwasaidia.

Mgogoro wa kina David Kafulila na Danda mpaka wakakimbilia NCCR-Mageuzi, vilevile ulianza na kumalizika bila CUF kuita wanahabari na kutangaziwa kwamba wanaunga mkono upande upi!

Kana kwamba haitoshi hata mwaka 2012 mgogoro



hivyo wanalijua hili!

Au kuna mwanasiasa yeyote kutoka Chadema, CUF, NCCR-Mageuzi, NLD, TLP au ACT-Wazalendo na vingine anayeweza kusema viongozi wao walizuiwa kufanya siasa au mikutano ya hadhara na wananchi?

**CHADEMA ILIVYOHUJUMU CUF YA LIPUMBA**

Wakati chama hiki cha Chadema kikitaka kuwaaminisha Watanzania kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inabinya demokrasia, wao ndiyo wamebobea kwenye hilo. Hakuna demokrasia ndani ya chama hicho kiasi kwamba Mbowe anaonekana kama kiongozi wa maisha. Baadhi ya watu walioonesha kukitaka kiti chake walikiona cha moto!

Lakini si hilo Chadema limekuwa kikituhumiwa kuwa na harakati ya kuhujumu vyama vingine vya upinzani kama vile uongozi wa chama hicho Kanda ya Pwani ulipoanzisha operesheni walioiita maalumu ya kusaidia Chama cha Wananchi (CUF) kumwondoa Mwenyekiti wake, Profesa Ibrahim Lipumba katika ofisi za Makao Makuu ya chama Chadema Kanda ya Pwani (jina tunalihifadhi), uamuzi wa chama hicho kusaidia CUF katika jitihada zake kumng'oa Lipumba ulilenga kunusuru CUF na Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) uliojumuisha Chadema, CUF, NCCR-Mageuzi, na NLD.

Kiongozi huyo bila aibu wala kificho aliwaambia waandishi wa habari katika ofisi za kanda hiyo, Dar es Salaam; "Sisi kama Chadema kwa umakini kabisa tutawasaidia viongozi wa CUF na wanachama wao kumwondoa msaliti ambaye ni Profesa Lipumba, Buguruni.

Nilijiuliza kuna nini kilijificha nyuma ya mpango ule uliohatarisha amani kwa Chadema kuingilia utendaji wa vyama vingine?

Kuna nani aliyefadhili upuuzi ule usiokubalika katika Taifa lolote linalojinasibu kuendesha mambo yake kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na demokrasia?

Chadema wameshawahi kuwa na migogoro ya uongozi mara nyingi, ukianzia ule wa mwaka 2004 ambao ulisababisha kundi kubwa la wanachama wakiongozwa na Dk. Paul Kyala na marehemu, uliowahusisha kina Profesa Kitila Mkumbo, Zitto Kabwe na hatimaye kufukuzwa chama, vilevile CUF haikuanzisha Operesheni yoyote ya kukinusuru Chadema kuwa na migogoro na makada wake mara kwa mara.

Ndiyo maana nauliza hizi kampeni za maandamano na operesheni hizi za Chadema za kila kukicha zina agenda gani nyuma yake?

Sawa tuwaachie wao na mamlaka, lakini nimemsikia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila akisema kwamba hiyo Januari 24 hili Jiji lake litakuwa kwenye Opresheni kubwa ya kufanya usafi ambayo itaambatana na askari wa Jeshi la Wananchi (JWTZ) wasiopungua 5000, askari wa Jeshi la Polisi wasiopungua 3000 na maofisa kadhaa wa Usalama wa Taifa sambamba na magari makubwa ya kubeba hizo 'taka' zitakazo zolewa!

Yangu macho, nasubiri kujionea hiyo safishasafisha ya Chalamila!

Kwa mawasiliano na mwandishi wa makala haya; 0784 122020/ 0768 888787.

Jamii

# Waandishi wana dhima kubwa kuipa taswira nzuri nchi yetu

**Na Felix Lugeiyamu**

KAZI mama ya kila mwandishi wa habari duniani ni kuhabarisha umma juu ya mambo kadha wa kadha. Kwa nyakati tofauti waandishi wanaweza kuendesha propaganda ili tu kufanikisha lengo.





Kwa muda sana suala la waandishi wa habari na dhana ya uzalendo hapa nchini limekuwa likifumbiwa macho. Kwa nyakati tofauti waandishi hapa nchini umeonekana kuandika habari zilizoegemea upande. Pengine inawezekana ni kutokana na sababu kadhaa ikiwemo kupungua kwa weledi na hapa vyuo vinavyotoa waandishi wa habari vinapaswa kunyooshewa kidole. Lakini pia unaweza kuwa tasnia yenyewe ilivyo kwamba ni kazi inayohitaji kuendana na muda hasa katika kuwasilisha habari kwa ajili ya uchapishaji au utangazaji.

Lakini ujio wa mitandao ya kijamii umesababisha kila mtu kudhani ni mwandishi wa habari. Anarusha tu kwenye mitandao kile anachodhani kinafaa kumbe kinaweza kuleta taharuki na athari kadha wa kadha.

Yote haya hayapaswi kuwa sababu ya kuvunja miiko ya uandishi wa habari.

Lakini pia kuna wakati uandishi wetu umekuwa ukijikitika zaidi kwenye habari zilizokaa kimbeambea badala ya kuhabarisha kwa kina masuala ya msingi kwa umma.

Je, inawezekana huku kukosekana kwa weledi katika tasnia ya uandishi wa habari ni kutokana na upungfu wa maadili kwa wahusika? Ni wazi kwamba tabia hii haipo kwa waandishi wote lakini kwa kiasi fulani hali ya kutowianisha habari (balancing), yaani kutoa haki sawa katika uandishi wa habari limekuwa tatizo sana.

Niliguswa na maneno ya mwenda zake, Hayati John Magufuli aliposema: "Vyombo vya habari mnajitahidi kutoa habari, lakini mtangulize uzalendo na haki kwa yule anayeandikiwa habari. Kumekuwa na uzushi sana mara fulani kafa (wakati siyo)... Ni mambo ya ajabu…

Lakini pia katika habari ambazo taifa letu linaandikwa vibaya watu wanashabikia, uzalendo umepungua tutanguliza uzalendo wa nchi yetu, niwaombe Watanzania wote tutangulize maslahi ya taifa, wajenga nchi ni sisi na wabomoa nchi ni sisi .

Wakati wa uongozi wake, vyombo vya habari vya mataifa makubwa vilikuwa kama vinaandika vibaya kuhusu nchi yetu. Hii inawezekana na nikutokana na baadhi ya wanasiasa kuisema vibaya nchi yetu kwa kuangalia maslahi yao binafsi. Lakini sisi waandishi wa habari tulikuwa na tunapaswa kuendelea kuwa makini na kuandika habari ambazo hazitachafua taswira ya nchi yetu.

Sasa hivi Chadema wamedai kwamba wanataka kuandamana wakipinga Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ambao umeshasomwa bungeni kwa mara ya kwanza. Kuna waandishi nina hakika watatumia hili kuchafua nchi yetu.

Kama waandishi kazi yetu ya msingi inapaswa kulisafisha taifa letu dhidi ya watu wanaoisema vibaya nchi yetu kwa mslahi yao ya kisiasa. Mara nyingi tumeonekana kuacha watu hao wazidi kulichafua taifa letu kana kwamba wanafanya vyema!

Maneno ya Hayati Magufuli yananikumbusha maneno ya Rais Mstaafu wa Kenya, Uhuru Kenyata aliposema "Lakini yako ni kwenda kuharibu jina la nchi yetu huko nje na mambo ambayo haina. Wazungu wamejaribu kutufunga kwa miaka sita wameshindwa. Wamesema hakuna kesi. Tosheka na haya. Na urudi tujenge Kenya yetu pamoja. Siyo kutuchafua kila saa. Tumechoka.

Hawajui ya kwamba kujenga ni ngumu lakini kupasua (kubomoa) ni dakika moja. Lakini hawana shida kubomoa kwa kuwa watatengeneza njia wawe viongozi. Uongozi siyo kiti bajameni, uongozi ni vile unawatedea wananchi ambao wataka kuongoza."

Dhana ya uzalendo ni pana sana na pengine inaweza kuwa ngumu kuielewa vyema. Lakini ifahamike kwamba mwandishi wa habari ana nguvu kubwa sana ya kusaidia katika kujenga na kukuza uzalendo dhidi ya Watanzania wote.

Badala ya kuruhusu watu wachafue nchi yetu inatupasa kama waandishi kuisafisha kila mara na kuinenea yaliyo mema na kufanya kila mmoja wetu atambue ubora wa nchi yake.

Hayati Magufuli alisema maneno mazito ya kwamba maendeleo ya nchi yetu na ujenzi wake uko mikononi mwa kila Mtanzania, sawa na Imani ya TANU na Azimio la Arusha. Ni wazi kwamba nchi yetu itandelea kwa sisi wenyewe kupambana na si kutegemea watu wengine.

Magufuli alisema, "Hakuna nchi moja duniani ambayo iko tayari kutupa misaada au mikopo au kuja kujenga viwanda katika nchi yetu kutimiza shabaha zake zote za maendeleo. Nchi zenye dhiki ni nyingi sana duniani. Na hata kama nchi zote zenye neema zingekubali kuzisaidia nchi zenye dhiki, bado ingekuwa msaada huo hautoshi. Lakini nchi zenye neema hazitakubali. Hata katika nchi ile ile, matajiri huwa hawatoi fedha zao kwa hiari ili zisaidie Serikali kuondoa dhiki."

Maneno haya yakatiliwa mkazo na Hayati Baba wa Taifa aliposema "Tutaijenga nchi hii kwa faida yetu wenyewe. Akipatikana mtu wa kutusaidia tutashukuru. Lakini kazi ya kujenga nchi hii kwa manufaa ya watanzania wote, ni kazi ya watanzania wenyewe. Si kazi ya mtu mwingine"

Suala la ujenzi wa nchi haliko mikononi mwa viongozi wa kubwa tu bali kwa kila mtanzania mmoja mmoja. Na watu wenye nafasi kubwa zaidi ya kufanikisha katika kuhamasisha maendeleo haya ni waandishi wa habari ambao huhabarisha umma. Nafikiri huu ni wakati mwafaka kwa kila Mtanzania kutanguliza uzalendo katika kutimiza majukumu yetu.

Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunawamaliza nguvu mabeberu kwa kuwa hawataweza tena kupitisha propaganda zao chafu dhidi ya viongozi wetu na taifa letu.

Naamini kiu ya Rais Samia Suluhu Hassan, kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake ni kuona kila Mtanzania kwa nafasi yake akiionea uchungu nchi yetu. Huu ndiyo wakati mwafaka wa kumuunga mkono Rais wetu katika jitihada zake za kuijenga nchi na Mungu atubariki.

*Mawasiliano ya mwandishi ni +255-71224-6001 flugeiyamu@gmail.com*

# Samia alivyomwaga mabilioni kuifungua Katavi kwa barabara

**Na Mwandishi Wetu, Katavi**

WALIOSEMA mtandao wa barabara katika nchi ni mithili ya mishipa ya damu katika mwili wa mwanadamu kutokana na umuhimu wake wa kuunganisha maeneo mbalimbali na kuboresha uchumi na maisha ya watu hawakukosea.

Kauli hii imedhihirika mkoani Katavi ambako serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imejenga barabara murua kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na kusababisha ziwe msaada mkubwa kwa ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja, mkoa huo na Tanzania kwa ujumla.

Kwa wanaokumbuka, Katavi ni moja ya mikoa mipya, hapo zamani baadhi ya wilaya zake zikiwa sehemu ya Mkoa wa Tabora na nyingine Rukwa, lakini mtandao wake wa barabara unaridhisha sana kwa sasa. Pongezi kwa Serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kumwaga fedha ili kuufungua mkoa huo anaotoka mtoto wa mkulima, Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda..

Saidi Juma (37), mkulima wa mpunga anayeishi kata ya Mbede, Wilaya ya Mpimbwe anasema, Tunalima sana zao la mpunga lakini tatizo lilikuwa jinsi ya kuutoa shambani na kuupeleka sokoni. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia kwa kutujengea Daraja la Msadya kwani daraja hilo ni muhimu sana kwa wakazi wa kata ya Chamalendi na Mbede na kwa uchumi wa Halmashauri ya Mpimbwe kwa ujumla," anasema.

Kukamilika kwa daraja hilo anasema kutawawezesha wananchi wa Chamalendi kusafirisha mazao yao hasa mpunga wanaoulima kwa wingi kuupeleka Maji Moto ambapo kuna soko kubwa la mpunga.

"Kimsingi, kukamilika kwa hili daraja kutafungua fursa kubwa ya kiuchumi na kijamii kwa wakazi wa maeneo yetu, anasema Said.

Kwa upande wake, Anna Masanja (43), mkazi wa Kitongoji cha Katonyaga kilichopo katika Wilaya ya Tanganyika, anaishukuru sana serikali kwa kuwafungulia barabara mbili; ya Kidongo Chekundu Katonyaga Kamsanga pamoja na Barabara ya Katuma Kahelele kwa kiwango cha changarawe.

"Barabara hizi kwetu ni muhimu sana kwa ajili ya usafirishaji wa mazao yetu ya mpunga. Kwa kufunguka barabara hizi maana yake ni kwamba sasa tuna soko kubwa na la uhakika la kuweza kuuza na kusafirisha mazao yetu muda wowote ule," anasema.

Innocent Mlay, meneja wa Tarura Mkoa wa Katavi anasema kwa hakika wameitekeleza vyema Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Kaulimbiu ya Tarura isemayo: 'Tunakufungulia barabara kufika kusikofikika kwa vitendo'.

Anasema katika miaka hii miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan wamefungua barabara ambazo hazijawahi kupitika tangia Tanzania ipate uhuru. Kwa sasa zinapitika na vivuko (madaraja) vimejengwa kwa wingi zaidi ili kuhakikisha kila mahali watu wanafika na kufanya shughuri zao.

Mlay anasema Chama Cha Mapinduzi kiliahidi kuimarisha fursa za ufikishaji mazao sokoni kwa kutengeneza barabara za vijijini na sehemu zenye uzalishaji na kwamba hilo limefanyika katika takribani kata zote mkoani humo.

"Mbali na barabara, tumejenga madaraja makubwa na madogo katika kila kata mkoani Katavi... Hilo tena si la kuuliza. Ukipita utajionea kwa macho yako mwenyewe. Sekta mbalimbali kama vile madini, utalii, mifugo, uvuvi na kilimo zinategemea ubora na uimara wa miundombinu ya barabara ili kuweza kukua kwa haraka na hivyo kuchangia pato la Taifa na mtu mmoja mmoja. Tumezifungua kwa upande wa barabara," anasema.

Mlay anasema Mkoa wa Katavi ni moja ya mikoa inayozalisha mpunga na mahindi kwa wingi. Anasema kasi ya ujenzi wa barabara bora za mijini na vijijini, zimesaidia sana wakulima na wafugaji kusafirisha mazao na mifugo kutoka mashambani na hivyo kupata manufaa makubwa ya kiuchumi.

Anasema mkoa huo kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 ulitengewa bajeti ya Sh. bilioni 13.3 kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara.

Kwa Wilaya ya Tanganyika Mlay anasema wametekeleza miradi mitatu; matengenezo ya barabara ya Kidongo Chekundu Katonyaga Kamsanga yenye urefu wa km 12, Katuma Kahelele urefu wa km 10 kwa kiwango cha changarawe ambapo matengenezo hayo yatagharimu jumla ya Sh. milioni 560,000,000 mpaka kukamilika kwake.

Mradi wa pili ni ujenzi wa Daraja Ifinsi lenye urefu wa mita 20 lililojengwa katika Mto Mnyamasi kwa gharama ya Sh. Milioni 866,084,344 na mradi wa tatu ni ujenzi wa madaraja madogomadogo mbayo yanajengwa katika barabara za mnyagala Mtakuja, Mnyagala Mwikangombe, Lupa Ntimba, Kidongo chekundu Katonyaga Kamsanga. Vivuko hivyo vinagharimi Sh. milioni 370,000,000.

Kwa upande wa Wilaya ya Mpanda Mlay anasema walipata mgao wa Sh. milioni 500,000,000 na kuielekeza kwenye kuipandisha hadhi barabara ya Mwamkulu yenye urefu km 6.5 kwa kiwango cha changarawe na matengenezo ya muda maalumu katika barabara ya Kasokola yenye urefu wa km 7.5

Katika jimbo la Nsimbo walipata mgao wa Sh. 1,614,000,000 ambapo katika Fedha hizo kiasi cha Sh. 324,000,000 wamezielekeza kwenye matengenezo ya barabara ya Ibindi Itenka A yenye urefu wa km 11.6 kwa kiwango cha changarawe pamoja na ujenzi wa kalavati katika barabara hiyo. Kiasi cha Shilingi Bilioni 1.29 wamezielekeza kwenye ujenzi wa madaraja mawili katika barabara ya Ibindi Itenka A na daraja moja katika barabara ya Itenka Mnadani ambapo mpaka sasa madaraja hayo yapo kwenye hatua ya upenzi yakinifu.

Kwa Wilaya ya Mlele yenye halmashauri mbili; Halmashauri ya Mlele pamoja na Halmashauri ya Mpimbwe, kwa mwaka wa Fedha wa 2022/2023 walitengewa kiasi cha Sh. Bilioni 4.8 kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali katika Halmashauri hizo.





## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala |0620 800 462

# Mmomonyoko wa maadili unatutesa hadi kwenye mitihani

PETER Masanja (si jina lake halisi) ni mtoto wa mfanyabishara mmoja wilaya moja pale Kanda ya Ziwa. Baba na mama yake, wakati tukio hili linajiri miaka ya 1980, wote wanajishughulisha na biashara.

Tangu akiwa darasa la kwanza hadi la saba hakuwa mwanafunzi 'aliyenyooka' vyema kulinganisha na wenzake.

Alikuwa mtoro wa mara kwa mara, mvivu wa kufanya kazi za darasani, mgovi, mvivu wa kujisomea na hata nidhamu yake haikuwa ya kuridhisha. Kutokana na hali hiyo, katika majaribio ya darasani hakuwa anafanya vizuri pia.

Licha ya kufikishiwa malalamiko na walimu kwamba pia ni bingwa wa matusi kwa wenzake, wazazi wa Peter hawakuwa wanachukua hatua stahiki; kumwonya, kufuatilia maendeleo yake darasani, kukagua madaftari yake, kuhakikisha anakwenda shule kila siku na hata kumwadhibu. Kikubwa 'ubize' wa kutafuta na kusahau jukumu lao la malezi uliwatawala!

Wazazi waliposhituka mtihani wa darasa la saba umefika na kwa kuwa walijua mtoto wao hana maandalizi mazuri ya kumwezesha kufaulu, wakaamua kufanya mbinu za udanganyifu ili mtoto ashinde mtihani na kuwashirikisha baadhi ya wazazi wenzao katika uovu huo!

Kilichotokea ni kwamba Baraza la Mitihani la Taifa liligundua uwepo wa udanganyifu katika darasa hilo na wanafunzi wote kufutiwa mtihani. Yaani ilikuwa mithili ya mtego wa panya ulionasa waliomo na wasiomo!

Kimsingi, wanafunzi kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vikuu hupata maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali kwenye taasisi mbalimbali za elimu wanazosoma.

Katika kufanikisha shughuli muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni au vyuoni, walimu wanao wajibu wa kufundisha wanafunzi huku wanafunzi kama Peter, wakiwa na wajibu wa kusikiliza na kuzingatia yale wanayofundishwa na walimu wao ili kuweza kupata yale wanayotarajiwa kujifunza.

Shughuli za ujifunzaji hutamatishwa na kupimwa kwa wanafunzi katika yale waliyojifunza. Upimaji huu huwa katika mfumo wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani ya kishule na kitaifa.

Upimaji katika mitihani hii hutoa taswira ya uelewa wa wanafunzi katika kipindi husika cha ujifunzaji wao. Mathalani; upimaji kitaifa darasa la nne, hutoa taswira ya uelewa wa wanafunzi katika yale waliyojifunza miaka minne yaani darasa la kwanza hadi la nne.

Kwa wanafunzi wa darasa la saba, hupimwa katika yale waliyojifunza katika kipindi chote cha miaka saba. Pia, upimaji kitaifa kidato cha pili hupima wanafunzi katika yale waliyojifunza katika kipindi cha miaka miwili, hali kadhalika kidato cha nne na sita.

Ili wanafunzi wafanye vyema katika mitihani hiyo, walimu wanao wajibu wa kuwaandaa vyema wanafunzi hao kwa kuwafundisha kikamilifu. Wana dhima pia ya kuhakikisha nidhamu kwa wanafunzi inasimama vyema.

Kwa upande mwingine wa shilingi, wanafunzi kama Peter wanawajibika kufanya kinachowekwa darasani, kusikiliza kwa umakini, kuuliza maswali pale ambapo somo halijaeleweka, kufanya mazoezi ya darasani na kujisomea vya kutosha ili kujiandaa vyema na mitihani hiyo na hatimaye kuweza kufanya vizuri ili kuendelea na ngazi nyingine ya masomo.

Wazazi pia kwa upande wao wana jukumu la kusimamia nidhamu ya watoto wao, kufuatilia nyendo zao ili kubaini kama kuna vitu vinaweza kuwafanya wasijifunze ipasavyo au kuwa na marafiki wa hovyo, kuwanunulia mahitaji muhimu ya kishule ikiwemo vitabu na mengine mfano wa hayo. Wazazi kama wa Peter, wanachangia uwepo wa watoto wasio na nidhamu.

### UDANGANYIFU KWENYE MITIHANI

Udanganyifu unaofanywa na wazazi kama hawa wa Peter umekuwa na madhara makubwa kwa watahiniwa wenyewe, kwa shule wanazosoma, kwa jamii nzima na hata kwa taifa.

Mtu anapofaulu kwa udanganyifu, kuna uwezekano kwamba anakwenda kuziba nafasi ya mwingine kwa sababu nafasi huwa ni chache.

Halikadhalika hatumtazamii afanye vizuri katika ngazi nyingine ya masomo anayoiendea. Hebu fikiria kama Peter kwa udanganyifu, kweli angefanya vizuri kwa masomo ya sekondari? Na kama ndio anatoka chuo, na kubahatika kuajiriwa, unadhani weledi na ufanisi wa Peter katika kazi utakuwa mzuri?

Jaalia Peter wetu huyu akapenyapenya kwa kuiba mitihani kwa sababu jasiri haachi asili hadi akawa daktari hospitali ya Mwananyamala. Mara paaap, uko mbele ya Dk. Peter Masanja unaumwa. Uliwahi kusikia habari ya daktari aliyetakiwa kumfanyia operesheni ya mguu mgonjwa yeye akamfanyia ya kichwa? Kama hujasikia, kwaheri!

Lakini baya zaidi udanganyifu husababisha wanafunzi kufutiwa matokeo yao kama ilivyokuwa kwa shule aliyokuwa akisoma Peter. Zipo shule ambazo hufutiwa hadi usajili kabisa!

Wakati wazazi wa Peter wanaweza kumpelekea mtoto wao shule ya kulipia, lakini wazazi wengi ambao ni wakulima katika shule aliyokuwa akisoma Peter hawakuwa na uwezo. Hebu fikiria madhila ya kuishia darasa la saba waliopata kwa sababu ya uovu wa mtu mmoja tu!

### UANDISHI WA MATUSI KWENYE MITIHANI YA KITAIFA

Zipo taarifa za baadhi ya watahiniwa wachache huandika lugha za matusi kwenye mitihani ya kitaifa. Jambo hili si ishara njema katika ujenzi wa taifa letu kwani watahiniwa hawa ni sehemu ya raia katika nchi yetu. Lakini wazazi siku hizi tunapokuwa 'bize' na kutafuta na kusahau majukumu tunachangia hali hii.

Kwanza, lugha ya matusi ni miongoni mwa tabia mbaya, ni jambo lisilokubalika kuanzia kwenye imani za dini hadi kwenye tamaduni zetu kijamii. Hata katika uga wa kisheria, matusi ni kosa la jinai, hivyo lugha ya matusi haikubaliki abadan asilani.

### MATOKEO YA DARASA LA NNE NA KIDATO CHA PILI KWA MWAKA 2023.

Akitangaza matokeo ya kitaifa ya upimaji wa darasa la nne na kidato cha pili, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (Necta), Dk. Said Mohamed amesema baraza limefuta matokeo kwa wanafunzi 178 wa darasa la nne na 28 wa kidato cha pili waliofanya udanganifu (jumla watahiniwa 206). Vilevile, baraza limewafutia matokeo wanafunzi watatu wa darasa la nne na 14 wa kidato cha pili (jumla watahiniwa 17) walioandika matusi kwenye karatasi za kujibia mitihani yao.

### TUHIMIZE UJENZI WA MAADILI MEMA KATIKA JAMII.

Pamoja na sababu kadhaa ambazo wataalamu wanaweza kuja nazo kama sababu zinazopelekea udanganyifu na uandishi wa matusi kwenye mitihani, lakini kubwa ninaloliona hapa ni mmomonyoko wa maadili.

Katika suala la udanganyifu kwenye mitihani, ni muhimu kwa wazazi au walezi, walimu na wanafunzi wenyewe kuzingatia maadili. Udanganyifu kwenye mitihani ni zao la mmomonyoko wa maadili kwani kwa wazazi, walimu na wanafunzi wenye maadili mema katu hawatakuwa sehemu ya kufanikisha njama za kufanya udanganyifu kutokana na kujua athari zake.

Uandishi wa matusi kwenye mitihani unaofanywa na baadhi ya watahiniwa wawapo kwenye vyumba vya mitihani, ni matokeo ya maadili mabaya waliyonayo baadhi ya wanafunzi. Mwanafunzi mwenye tabia njema, hawezi kuandika matusi kwenye mitihani. Ni muhimu kwa wazazi na walezi kuwajenga watoto wao kwenye maadili mazuri ili waepukane na tabia mbaya ikiwemo hii ya kundika matusi kwenye mitihani ya kitaifa.

Walimu kwa upande wao, wanayo fursa ya kuzuia uandishi wa matusi kwa kuwakumbusha mara kwa mara wanafunzi kuepukana na tabia hii mbaya. Wawakumbushe umuhimu wa kuzingatia maelekezo ya kwenye mitihani badala ya kufanya vitu visivyokubalika. Kimsingi, mwanafunzi aliyejiandaa vyema kwenye mitihani kamwe hawezi kuandika matusi kwani malengo yake ni kufanya vizuri ili avuke ngazi nyingine.

Ni muhimu wanafunzi wakakumbushwa kuwa hata kama wamekosa majibu ya kujaza kwenye karatasi zao za kujibia, waepuke kuandika matusi kwa sababu ni afadhali kufeli mtihani kuliko kufutiwa matokeo kwa kuandika matusi.

Tuzingatie hili kwamba kuanzia ngazi ya familia, ukoo, jamii, kata, tarafa, wilaya, mkoa hadi taifa tunalo jukumu kubwa la ujenzi wa maadili mema katika jamii.

Tukiwa na jamii yenye maadili mema, tukawalea vyema akina Peter, udanganyifu na matusi kwenye mitihani pamoja na tabia nyingine nyingi mbaya na zenye ukakasi zitatoweka.

*Dk. Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni (+255) 620 800 462.*





Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Misumari ya mahusiano - 2

Wiki iliyopita tulianza kuliangalia somo hili ambalo lina makusudi ya kuimarisha mahusiano yetu. Mambo haya inawezekana unayachukulia kirahisi au kutoyapa uzito lakini ukiyazingatia na kujilazimisha kuyafanya ndiyo huleta uimara wa mahusiano na kuwajengea furaha walio kwenye mahusian.

Amani, uimara na furaha kwenye mahusiano hujengwa kwa mtu kuamua kwa dhati kufanya mambo haya. Karibu kwenye safu hii kwa faida yako na ustawi wa jamii yetu.

Wiki iliyopita tuliangalia mambo manne na leo tunaendelea na mengine ambayo hatukuyagusia.

**5. KUMPA CHANGAMOTO / KUMHAMASISHA KUWA BORA**

Mtu anataka mwenza anayeweza kum-challenge na kumpa hamasa ili kuwa mtu bora zaid. Fanya jambo hili kwa ustaarabu bila vitisho au kutweza utu wake. Mpe hamasa mwenzi wako kuwa toleo bora zaidi la yeye mwenyewe kwa ku -"adopt" mambo yatakayombadilisha taratibu.

Kwenye mchakato huu nenda naye taratibu hata kwa wewe pia kufanya anavyotakiwa kufanya ili ionekane kuwa ni ninyi kwa pamoja.

Hitaji hili ni kubwa zaidi kwa mwanaume. Kwenye mahusiano mwanaume anahitaji mwanamke mwenye hamasa kubwa kumfanya mwanaume huyo kuwa bora na mwenye mafanikio tofauti na jana yake.

Ikiwa kwa sababu yoyote unafikiri anaishi chini ya uwezo wake, nenda kwa Mungu kwa maombi mwombee kwanza na pia omba hekima ya kumwongoza kwa upole kuelekea kwenye njia sahihi.

**7. KUMSIFIA (COMPLIMENT)**

Hili ni moja ya jambo muhimu kwa mwenzi. Kumsifia ni kuonesha kwamba umeona na kuzingatia. Inaonesha kuwa kuna kitu cha ziada umeona kwake, inaonesha kuwa si kawaida.

Hii inampa nguvu, kujiamini na hamasa ya kufanya zaidi. Watu wengi hawajui kuwa kwenye mchakato wa kumbadilisha mtu au kumfanya kuwa bora, sifa ni muhimu kuliko lawama na dharau.

Pamoja na kwamba hili linahitajika pande zote za mahusiano, jambo hili ni muhimu zaidi kwa mwanamke. Yeye kama tulivyoona wiki iliyopita, anahitaji kujua kuwa unamzingatia (Attention). Sasa kusifiwa ni muhimu kwake.

Mwanamke hachoki kupata sifa, na ukitaka furaha yako kupitia yeye basi mpe sifa kwa kadiri unavyoweza lakini angalizo ni moja tu, usimsifie uongo kama leo kafanya vibaya onesha kuwa unatambua siku zote yeye ni bora kwenye eneo hili. Hii inatosha.

**8. KUJITOA KWAKE (DEVOTING)**

Mahusiano yanahusha dhana ya kujitoa kwa mtu, unajitoa kwa mwenzi wako kabisa. Jiweke wazi kufanya maisha yake kuwa bora kila wakati, simama naye katika raha na shida, ni muhimu uhakikishe anaona kwamba yeye ndiye mtu muhimu zaidi kwenye maisha yako.

Unapojitolea kwake, bila kujali vikwazo vinavyokujia maishani kama vile kazi au watoto, utapata njia ya kumpa umakini wako kamili. Kwa ufupi, jifunze kumfanya awe "kila kitu" kwako kila wakati.

Pamoja na kuwa hili ni jambo muhimu kwa kila mmoja, lakini hili ni muhimu zaidi kwa mwanaume. Mwanamke anatakiwa kujitoa kwa asilimia zote kwa mwenzi wake.

Si vyema mwanamke kuonesha hali ya kujitegemea kwa asilimia mia moja kwenye mahusiano. Kila mwenzi kujitegemea inapunguza mshikamano (bond) baina ya wenzi wawili.

**9. HAMU/SHAUKU (DESIRE)**

Mtu anayetamani kitu kama vile simu janja au gari jipya, anaelewa dhana ya hamu. Unapohitaji kitu kwa hamu, utafanya kila juhudi kukipata.

Kwenye mahusiano dhana hii huwa inaonekana sana mwanzoni mwa mapenzi. Ndiyo maana kipindi hiki kinakuwaga bora. Mahusiano yanahitaji kila mmoja kuwa na shauku na hamu na mwenzi wake.

Huwa nafundisha somo muhimu linaitwa "LAWS AND ORDER" kwenye somo hilo kuna kanuni inaitwa The Law of Persuit". Kanuni hii inawataka wenzi kuendeleza ile hali ya kuoneshana mambo mazuri uliyokuwa unayafanya wakati unamwonesha mwenzi wako kuwa unamhitaji katika maisha yako.

Pamoja na kuwa hili ni muhimu kwa wote, wanawake wanahitaji kutamaniwa na wanataka waonyeshwe hilo zaidi. Mkeo au msichana uliye naye anataka uwe na hamu ya kumtamani hata kama mmeshaoana kwa miaka mingi.

Ikiwa kwa sababu yoyote unafikiri anaishi chini ya uwezo wake, nenda kwa Mungu kwa maombi mwombee kwanza na pia omba hekima ya kumwongoza kwa upole kuelekea kwenye njia sahihi.

Mshike, mpe busu, na anzisha mapenzi. Usingoje daima yeye ndiye anayekujia; mwoneshe mkeo bila shaka kwamba bado unavutiwa naye.

**10. KUTIA MOYO NA KUTOA HAMASA (ENCOURAGEMENT)**

Kila mtu anahitaji kuhamasishwa na kutiwa moyo kusonga mbele kwenye maisha. Natambua wanaume pamoja na uimara wao, hili ni hitaji lao la msingi.

Usidanganyike na tabia yake ya kiume, wewe kama mke wake, unapaswa kuwa shabiki wake nambari moja na mshangiliaji wake mwenye shauku zaidi.

Mtie moyo na mhamasishe hata wakati wa nyakati ngumu; Ninaposema nyakati ngumu ni pamoja na zile za kushindwa au kukosea na hata kupotea kwa namna moja au nyingine. Hata nyakati hizo mwambie kuwa upo naye kila hatua ya njia yake ukimsaidia na kumwombea mpaka ashinde.

Wework Consult - Your Partner in Growth.

**Itaendelea wiki ijayo…**





Na Hamisi Kibari

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 15

**Baada ya kuthibitishiwa na daktari kwamba mkewe amefariki dunia kutokana na kipigo alichomshushia, Chris anashirikiana na daktari kuficha kifo cha mkewe akidai ametoweka na hajui alipo. Anaahidi kumsaka. Daktari anaahidi kushughulikia kila kitu na kuondoa katika makabrasha yote hospitalini jina la mkewe. Hata hivyo, gharama za kufanikisha hilo ni kubwa na zinasababisha daktari atwae nyumba ya Chris. Mwanaume huyo ambaye biashara yake ya kuuza mbao na vifaa vya ujenzi ilikuwa inakwenda vyema ghagla inachungulia kaburi. Haya yote ni tangu alipokutana na mrembo aliyekuwa akitikisa mji wa Tabora, Joyce na kuanzisha uhusiano naye. Baada ya kumfilisi, Joyce anamkataa Chris na kugeukia kwa mwanaume mwingine na kusababisha Chris afanye fujo kubwa ya kumpinga Joyce na huyo mpenzi wake mpya na sasa anatafautwa na polisi... Endelea.**

"Shikamoo Mzee Mahmoud," Mwalimu Misango alimsalimia mzee huyo mwenye mchanganyiko wa damu ya Kiarabu na Kibantu. Alikuwa Mzee maarufu mjini Tabora."Marahaba, karibu.""Samahani, nilikuwa ninamuuliza huyu mpangaji wako, Chris Magati. mbona banda halina uhai?"

"Ah! Ni yule dada yake... Nilianza kukusahau mwalimu. Uzee unakuja kwa kasi."

"Ni Mimi baba.""Nina muda mrefu simwoni na sina habari yoyote kutoka kwake. Mimi binafsi ninamtafuta sana. Ninaumwa na hajanilipa kodi miezi sita sasa... Nilidhani wewe dadake ungenisaidia kujua aliko?""Sijui alipo. Ina maana huna tetesi zozote kuhusu mahala alipo?""Tena ningepajua ingekuwa vyema... Kitu kingine ni kwamba huyu kijana sijui kafanya nini huko. Toka wiki iliyopita askari polisi wanakuja kumtafuta hapa mara kwa mara. Anauweka huu mtaa katika msukosuko mkubwa. Watu wananiuliza maswali nashindwa hata kujibu. Kwani kafanya nini huko?""Hata mimi sijui. Nimesikia polisi wakimtafuta ndio maana na mimi nimekuja hapa kuona kama nyinyi mna habari zake zozote.""Mimi sina habari yoyote kuhusu mdogo wako... Tena mwezi huu ukiisha bila kumwona, nitaomba kibali cha polisi, nivunje duka lake nipangishe mtu mwingine na kushika mali zake kufidia gharama zangu ingawa naona kafilisika. Hata sijui kama kuna kitu cha kufidia kodi yangu ninayodai.""Haya baba mimi ninakwenda.""Sawa, lakini ikiwa utamwona, mpe hayo maelezo yangu. Mwisho wa mwezi ninavunja kisha naleta mpangaji mwingine.""Sawa baba," Mwalimu Misango alijibu akiondoka. Aliamua kwenda nyumbani kwa binti aliyekuwa akimuuzia Chris duka, Diana Masemele ili kuona kama anaweza kupata habari zozote kuhusu mdogo wake. Mwalimu alikuwa amejaribu mara kadhaa kumtafuta binti huyo kwa namba ya simu aliyokuwa nayo lakini ilionekana kama haitumii tena.

Hata hivyo, alikuwa hakumbuki vizuri nyumba aliyokua akiishi. Kwa kuwa alikuwa akijua mtaa, Buzebazeba, aliitafuta huku akiulizauliza na kufanikiwa kumpata akiuza genge nje ya nyumba yao.

"He! Siku hizi umefungua genge ama unamuuzia mama yako?" Aliuliza Mwaimu Misango."Ndio, nimefungua genge... Karibu sana, mwalimu. Unadhani nitaendesha vipi maisha yangu kama sikujishughulisha na biashara kama hizi!""Vipi kumetokea nini. Mbona banda la biashara mmefunga?""Mwalimu usin'chekeshe. Yaani unaniuliza mimi kuhusu banda wakati nina karibu mwezi sasa nikiwa sijui kinachoendelea huko? Mara ya mwisho si ulikuja nikakueleza namna hali ilivyo mbaya nikadhani utamweka chini mdogo wako lakini hali ikazidi kuwa mbaya. Kulikuwa hakuna tena cha kuuza pale bandani.""Sijawahi kukutana naye na sina habari kabisa na mahala alipo. Mwanzoni alikuwa hapokei simu yangu lakini sasa namba za simu zake zote nilizo nazo inaonekana kama kabadilisha. Ni kama wewe, tangu majuzi ninakutafuta lakini sikupati kwenye simu.""Simu yangu ilipotea. Nimepata nyingine lakini nimerejesha line moja tu nyingine sijaresha na nadhani ndio ambayo ulikuwa nayo. Kimsingi, biashara ilishindikana baada ya mali bandani kuisha kabisa. Kama nilivyokuelekeza siku ile, mdogo wake na yule mwanamke kila siku wanachukua pesa tu na kwenda kutumbua. Kila nikiuza jioni pesa yote inaondoka. Hakuna mali mpya inayoingia. Hapo kuna biashara tena? Na siku ile nilisita tu kukuambia lakini ninadai mishahara ya miezi mitatu. Siku za mwisho nilikuwa ninasaidiwa kuendesha maisha na mchumba wangu. Ninafikiria kufungua kesi kumshitaki mdogo wako nidai ujirfa wangu."

"Duh! Pole sana Diana… Yaani!"

"Mwalimu, nimeendesha maisha kwa shida sana huku mdogo wako akitumbua tu pesa na huyo hawara yake. Tuseme mkewe ndio kamkimbia kabisa?"

"Mkewe tangu ametoweka hajulikani alipo. Hata mimi nimeanza kuwa na wasiwasi ingawa nilimsikia mara kadhaa akisema anaweza kuamua kumlipizia kisasi mumewe kwa maana na yeye kutafuta bwana. Tena alikuwa akisema bila kunificha kwamba mabwana wanaomtaka, hadi wengine kumshawishi aachike kwenye ndoa ili wamuoe hata kama keshazaa watoto wawili. Mimi nikawa ninamwambia wanakudanganya tu. Hayo mawazo kwamba anaweza kuwa kafuchwa na bwana  sasa yametoweka kwa sababu hii sasa si kawaida. Yaani imekuwa shida juu ya shida. Sasa ni zaidi ya miezi nane na mimi ndiye ninayehangaika na watoto wao. Nilijua pengine unajua mahala alipo.""Kwa kweli sijui.""Haya Diana, Kwa heri," alisema Mwalimu Misango akiondoka kinyonge.

* * *

Mwalimu Misango alimpakata Huba ambaye alikwenda kumshitakia huku akilia baada ya kukorofishana na kaka yake Kenny, wakati wakicheza jioni hiyo.

Mwalimu alihisi Huba ameanza kupata joto baada kupitisha kiganja chake cha mkono wa kulia kwa nyuma kusikiliza joto la mtoto huyo ambaye alikuwa akiendelea kulia. Usiku ulioipisha usiku Huba alilala na homa, Mwalimu akampa dawa za kutuliza maumivu lakini kulipokucha asubuhi, na hadi Mwalimu anakwenda kazini, mtoto huyo wa miaka mitatu na nusu alikuwa anaendelea vizuri.

Licha ya msichana wa kazi kumjulisha kwa simu kwamba Huba alikuwa anaendelea vizuri akicheza kama kawaida, Mwalimu Misango aliomba ruhusa mapema kazini ili kuja kuangalia maendeleo ya hali yake.

Tofauti na mchana wakati anafika, sasa joto lilianza tena kupanda.

"Nyamaza Huba, nitamchapa Kenny kwa uchokozi," alisema Mwalimu Misango akipanga kumpigia mumewe simu asipitie kokote jioni hiyo akitoka kazini ili wampeleke hospitali Huba.

"Mtoto analia nini, au amemkumbuka mama yake. Bado hajazoea tu?" Alihoji mumewe ambaye alikuwa anaingia nyumbani jioni hiyo akitokea kazini.

"Kachokozana na kaka yake. Kimsingi Huba ameanza kumsahau mama yake... Isipokuwa ameanza kuchemka tena. Nilikuwa ninapanga kukupigia simu ili uwahi tumpeleke hospitali jioni hii."

"Sawa. Yaani mama mtu ameamua kuuchuna kabisa huko aliko? Mama gani unatelekeza watoto ili kulipa kisasi kwa mume wako?"

"Hilo nalo nilitaka tulijadili Baba Kessy. Hali hii si ya kawaida. Kwa nini mama mtu kama bado yuko hai asimkumbuke mwanae?" Alihoji Mwalimu Misango. Mumewe aliyekuwa amesimama karibu yake akabaki kimya.

Mwalimu akaendelea: "Hata baba mtu, hapo nyuma ukiona katuma meseji ni ya kuuliza watoto wake. Ukiona katuma pesa ni kusaidia malezi ya wanawe, naye miezi miwili sasa kimya. Hajulikani alipo, simu zake hazipatikani wala nini. Si Hali ya kawaida na hatuwezi kubaki kimya."

"Unashauri tufanyeje?"

"Kinachonishangaza hata Jacob na baba yake mdogo wamekaa kimya. Mara ya mwisho nilipoongea na Jacob kumjulisha yaliyomkuta shemeji yake, majibu yake kidogo yalinishangaza. Alisema wao sasa wamemwachia Mungu hawataki kupoteza muda wala kusikia kabisa habari za Baba Kenny. Majibu gani hayo sasa?"

"Hujajibu swali langu. Tufanyeje?"

"Nilikuwa nashauri twende polisi kutoa taarifa kuhusu kupotea kwa Baba Kenny halafu ikiwezekana tutoe picha zao wote wanandoa kwenye magazeti."

"Hilo wazo ninakubaliana nalo," alisema Misango na mara simu ya Mwalimu Misango ikaita.

Akiwa bado amempakata Huba ambaye sasa linyamaza, akapokea simu ambayo ilikuja bila kuonesha jina la mpigaji.

"Hallo, habari," iliuliza sauti ya kike.

"Nzuri."

"Nazungumza na Mwalimu Misango?"

"Ndiyo. Nani mwenzangu."

"Naitwa Maua, maarufu Mama Jane. Ninaishi Muhogoni, hapa jirani tu na alipokuwa akiishi Mama Kenny."

"Tunafahamiana?"

"Mimi ninakufahamu lakini nadhani wewe hunifahamu."

"Unasemaje Maua."

"Nilikuwa nina habari zinazomhusu wifi yako, Mama Kenny. Nilikuja shuleni ili tuzungumze lakini nimekuta umeshaondoka. Nimeambiwa leo umeondoka mapema ndio nikapata namba yako ya simu."

Maneno yake yalimshitua Mwalimu Misango. Akahisi mapigo ya moyo yanabadilika.

"Habari za Mama Kenny kama unazo nina hamu sana kuzisikia. Nzuri mbaya?"

"Mchanganyiko?"

Jibu hilo lilizidi kumchanganya Mwalimu Misango.

*Itaendelea*

> **Mkewe tangu ametoweka hajulikani alipo. Hata mimi nimeanza kuwa na wasiwasi ingawa nilimsikia mara kadhaa akisema anaweza kuamua kumlipizia kisasi mumewe kwa maana na yeye kutafuta bwana.**

VITA VYA ISRAEL, HAMAS:

# Video ya Hamas yadaiwa kuonyesha mateka wafu

**YERUSALEM, Israel**

ITAI Svirsky, ametajwa kuwa mmoja wa mateka wawili wa kiume walioonyeshwa kwenye picha za hivi majuzi zilizotolewa na Hamas.

Kundi la Hamas limetoa video mpya inayodaiwa kuonyesha miili ya mateka wawili wa Israel, huku wanamgambo hao wakidai kuwa walikufa katika mashambulizi ya anga huko Gaza.

Hii inakuja siku moja baada ya Hamas kutoa video nyingine ya mateka hao walipokuwa hai, lakini ikionya kuwa wanaweza kufa iwapo Israel itaendelea na mashambulizi yake ya mabomu.

Israel ilikanusha kuwa waliuawa mashambulizi.

Waziri wake wa ulinzi aliwashutumu wanamgambo hao kwa unyanyasaji wa kisaikolojia.

Aliongeza kuwa shinikizo la kijeshi ni muhimu ili kuwaachilia mateka zaidi.

Video hiyo iliyotolewa juzi Jumatatu inamuonyesha mwanamke, Noa Argamani, akizungumza kwa kulazimishwa na kusema kwamba wanaume wawili ambao alikuwa amefungwa nao waliuawa wakiwa wametekwa.

Anasema wanaume hao ambaye mmoja wao alitambuliwa kama Itay Svirsky (38), waliuawa na shambulio letu wenyewe la IDF, akimaanisha Jeshi la Ulinzi la Israel.

BBC.




## Marekani yailaani Iran mashambulizi kwa Iraq

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imeilaani Iran kutokana na mashambulizi ya makombora karibu na mji wa Irbil Kaskazini mwa Iraq na kuyataja kuwa mashambulio ya kizembe na yasiyostahili. "

Kikosi cha Iran Revolutionary Guards, kilisema kilishambulia kile walichodai kuwa ni makao makuu ya kijasusi ya Israel Kaskazini mwa Iraq kwa makombora ya balestiki.

Watu wanne waliuawa na wengine sita kujeruhiwa katika shambulio la Jumatatu iliyopita, kwa mujibu wa Baraza la Usalama la Kurdistan nchini Iraq.

Iraq ilishutumu mashambulizi hayo na kuyataja kuwa ni ukiukaji wa uhuru wake.

Mashambulizi hayo yanakuja huku kukiwa na mvutano unaoongezeka katika eneo hilo tangu vita vya Israel na Hamas kuanza Agosti 7, mwaka jana.

Mzozo huo umezidi kuanza kutapakaa na kuhusisha washirika wa Iran kutoka Lebanon, Syria, Iraq na Yemen.

"Tutaendelea kutathmini hali ilivyo, lakini dalili za awali zinaonyesha kwamba hii ilikuwa shambulio la kizembe na isiyo sahihi," Adrienne Watson, Msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa la White House, alisema katika taarifa.

BBC.

> **Tutaendelea kutathmini hali ilivyo, lakini dalili za awali zinaonyesha kwamba hii ilikuwa shambulio la kizembe na isiyo sahihi**

VITISHO DHIDI YA MAJAJI KENYA:

# Jaji Mkuu ataka mazungumzo na Rais Ruto

**NAIROBI, Kenya**

JAJI Mkuu wa Kenya, Martha Koome, anasema Idara ya Mahakama imemwandikia barua Rais William Ruto, kutaka kushughulikia masuala aliyoibua kuhusu baadhi ya majaji.

Rais Ruto katika siku za hivi majuzi, alizusha vita dhidi ya Idara ya Mahakama, akiwashutumu baadhi ya majaji wafisadi ambao hawakutajwa kwa kushirikiana na upinzani kuzuia miradi ya serikali yake.

Akihutubia mkutano na wanahabari juzi Jumatatu, Koome alisema mashambulizi dhidi ya mahakama, yanatishia kuifanya nchi kuwa na machafuko .

"Iwapo mwelekeo huu utaachwa kuendelea bila kusitishwa, tuko kwenye ukingo wa mgogoro wa kikatiba ambao unaweza kusababisha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, alisema Koome na kuongeza:

"Kwa hivyo, tutalenga kufanya mazungumzo hayo, tumeandika barua na ninaamini kuwa Rais atatupa muda."

Kiongozi wa upinzani, Raila Odinga, amemkashifu Rais Ruto kwa kujaribu kuwatisha majaji huku kundi la mawakili likifanya maandamano wiki jana kulaani mashambulizi ya Rais.

Rais Ruto aliyeingia madarakani Septemba, 2022, amekosolewa kwa kuanzisha ushuru mpya huku gharama ya maisha ikipanda.

Kodi mbili mpya ushuru wa nyumba na makato ya bima ya afya kwa wote zimepingwa mahakamani na uamuzi unasubiriwa. BBC.



## Donald Trump kushinda kura za wajumbe wa Republican Iowa

**WASHINGTON, Mareklani**

DONALD Trump, anatarajiwa kushinda Uchaguzi Mkuu wa chama cha Republican cha Iowa, kulingana na CBS News.

Mshirika wa BBC wa Marekani CBS News anakadiria kuwa Donald Trump atashinda takriban wajumbe 16 huko Iowa.

Iowa ina wajumbe 40 wa chama cha Republican.

Haya ni makadirio ya haraka na inatoa dalili kali ya nguvu ya Trump katika chama hicho. .

Kura bado zinahesabiwa , huku kaunti 11 pekee kati ya 99 za Iowa zimeripoti matokeo hadi sasa.

Kura za maoni za CBS News zilionyesha Trump akipokea uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa Waevanjelisti wa kizungu na wapiga kura wahafidhina, kambi kuu za wapiga kura ambazo hazikuwa na hakika na sifa zake mwaka 2016. BBC.



# Kombora la Wahouthi laipiga meli ya mizigo ya Marekani

**SANA'A, Yemen**

WAASI wa Houthi, wameishambulia meli ya mizigo inayomilikiwa na Marekani kwa kombora la balestiki katika pwani ya Yemen, Marekani imesema.

Maafisa wa meli hiyo, Gibraltar Eagle, waliripoti kuwa hakuna majeraha au uharibifu mkubwa, kwa mujibu wa Kamandi ya Jeshi la Marekani katika eneo la Mashariki ya Kati (Centcom).

Meli hiyo yenye bendera ya Visiwa vya Marshall inaendelea na safari katika Ghuba ya Aden.

Wahouthi wanaoungwa mkono na Iran, wamekuwa wakishambulia meli tangu Novemba, mwaka jana kupinga vita vya Israel dhidi ya Hamas.

Kampuni ya usafirishaji ya Eagle Bulk Shipping, ilisema kuwa shehena hiyo kubwa ilikuwa imebeba bidhaa za chuma na ilikuwa umbali wa takriban kilomita 160 nje ya pwani katika Ghuba ya Aden ilipopigwa na kombora.

Ilisema meli hiyo ilipata uharibifu mdogo kwenye sehemu ya kubebea mizigo, lakini iko imara na inaelekea nje ya eneo hilo.

Saa kadhaa kabla ya shambulio hilo, Centcom ilisema kuwa kombora lingine lililorushwa kuelekea upande wa Marekani katika Bahari ya Shamu, lilinaswa na kuangushwa na ndege ya kivita ya Marekani.

Wahouthi wamekuwa wakishambulia meli za kibiashara katika Bahari ya Shamu ambazo kundi hilo linasema kuwa zina uhusiano na Israel, au kuelekea kwenye bandari za Israel.

Inasema mashambulizi hayo yanaonesha lengo lao la kuwaunga mkono Wapalestina na Hamas katika vita vinavyoendelea Gaza, huku Israel ikiendelea huko na harakati zake za kijeshi.

# Wafahamu Wafungaji bora wa muda wote wa AFCON



**Na Valensi Mbaga**

MICHUANO ya Kombe la Mataifa ya Afrika yamerejea tena mwanzoni mwa 2024 huku kukiwa na nafasi kwa timu nyingi za Taifa kufanya vizuri na kunyakua kikombe hicho.

Katika historia zilikuwepo nyakati nzuri ambazo mashabiki wangi wa soka walizifurahia huku baadhi ya majina mashuhuri katika soka la Afrika yakiwa makubwa zaidi katika historia ya mashindano hayo.

Mashindano haya ya 2024 yatashirikisha baadhi ya nyota wa dunia akiwemo Mohamed Salah, Victor Osimhen na Sadio Mane, huku swali kubwa ni kuhusu tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwenda kwa nyota gani pamoja na mafanikio ya timu kwa ujumla.

Ifuatayo ni taarifa kamili kuhusu wafungaji bora wa muda wote wa AFCON, washindi wa Kiatu cha Dhahabu na njia walizopitia kufikia malengo hayo.





**1: Samue Eto'o | Cameroon| mabao 18**

Kwa sasa ndiye mfungaji bora zaidi lakini hadi toleo la 2008 la Kombe la Mataifa ya Afrika, Samuel Eto'o alishinda tuzo hiyo mwaka wa 2000 na 2002. Alikuwa mfungaji bora pamoja mwaka wa 2006 na kutwaa Kiatu cha Dhahabu mwaka wa 2008.

**2: Laurent Pokou | Ivory Coast | mabao 14**

Huyu ni Mshindi mara mbili wa Kiatu cha Dhahabu mwaka 1968 na 1970, akiwa na jumla ya mabao 14 katika mechi nane kwenye matoleo ya mfululizo ya AFCON, ikiwa ni pamoja na kupachika mabao matano katika mchezo dhidi ya Ethiopia.

**3: Rashidi Yekini | Nigeria | mabao 13**

Mchezaji wa Nigeria Rashidi Yekini alikuwa mfungaji bora katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika 1992 na 1994, akishinda michuano hiyo mwaka 1994.

**4: Hassan El-Shazly | Misri | mabao 12**

Kombe la Mataifa ya Afrika la 1963 lilishuhudia El-Shazly akikusanya mabao sita. Aidha, mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri alifunga mabao mengine sita kwenye michuano hiyo ya AFCON

>>Inaendelea uk. 21

# Wafahamu Wafungaji bora wa muda wote wa AFCON







>>Inatoka uk. 20

**5: Patrick Mboma | Cameroon | mabao 11**

Baada ya kushinda medali ya dhahabu katika fainali ya Olimpiki ya Sydney 2000 dhidi ya Uhispania, aliibuka mfungaji bora kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika la 2022 na 2004. Bila kusahau, Mboma aliisaidia Cameroon kutwaa ubingwa wa AFCON mnamo 2000 na 2002.

**6: Hossam Hassan | Misri | mabao 11**

Mbali na mabao 11 katika michuano hiyo, Hassan alishinda kiatu cha dhahabu akiwa na Misri katika misimu ya 1986, 1998 na 2006. Hasa, katika Kombe la AFCON 1998, Hassan alikuwa mfungaji bora wa akiwa na mabao saba. Hapo ndipo alipofunga hat-trick dhidi ya Zambia na mabao mawili katika nusu fainali dhidi ya wenyeji Burkina Faso.

**7: Didier Drogba | Ivory Coast | mabao 11**

Fowadi huyo wa zamani wa Chelsea aliishia kuwa mshindi wa pili katika misimu ya 2006 na 2012 ya michuano hiyo ambapo alifunga mara tatu kila moja.lakini pamoja na hayo anasimama kuwa moja kati ya wafungaji mashuhuri na shujaa wa taifa lake.

**8: Ndaye Mulamba | DR Congo | mabao 10**

Akiwa na mabao 10 kwenye michuano hiyo, Mulamba alifunga rekodi ya mabao tisa katika msimu mmoja mwaka 1994. Alikamilisha kazi hiyo katika michezo sita pekee na kuiwezesha Zaire ya wakati huo (sasa DR Congo) kutwaa taji hilo, pamoja na mabao mawili dhidi ya wenyeji Misri katika nusu fainali.

**9: Kalusha Bwalya | Zambia | mabao 10**

Hatima alikuwa na jukumu la kucheza kwani Bwalya alikosa ndege mnamo 1993 ambayo ilianguka na kuua wachezaji wengi wa timu ya taifa ya Zambia. Kupitia mchuano uliogusa nyoyo za mashabiki wengi mnamo 1994, mshambuliaji huyo aliiongoza timu yake hadi fainali kama nahodha.

Maarufu kama "Kalusha", alikuwa mfungaji bora katika mashindano yaliyofuata ya AFCON akiwa na mabao matano na baadaye akateuliwa kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia wa FIFA.

**10: Mengistu Worku | Ethiopia | mabao 10**

Aliisaidia Ethiopia kutwaa ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka wa 1962, alichangia kama mfungaji bora akiwa na mabao matatu. Worku anasalia kuwa mfungaji bora zaidi nchini akiwa na mabao 10 katika matoleo sita ambayo alikuwa sehemu yake.

Swali linabaki kuwa Je? Ni nan ataungana na mashujaa hawa katika vitabu vya kihistoria na tumeshaanza kuona mapinduzi makubwa katika soka la bara la Africa.







# Sio tu mpira na tamaduni zipo

**YAMOUSSOUKRO,Ivory Coast**

YAPO mambo mengi ya kushangaza katika Michuano ya AFCON msimu huu lakini kubwa kabisa ni namna walivyoonyesha mitindo ambayo imedumisha tamaduni zao lakini pia namna mataifa makubwa katika historia yanavyokutana na upinzani mkubwa na hata kupoteza alama tatu katika mzunguko huu wa kwanza.

Kipekee ubunifu wa mavazi unatangaza Tamaduni na ni moja kati ya kitu kikubwa kilichoipamba michuano hii.Timu ya taifa ya Ghana, inayojulikana kama Black Stars, ilitoa kauli muhimu ya kitamaduni ilipowasili. Kwa kukumbatia urithi wao, timu ilivalia mavazi ya kitamaduni ya Kente.

Kama taifa mwenyeji Ivory Coast sio tu imekuwa muhimu katika mashindano hayo lakini pia katika kuonyesha fahari ya kitaifa kupitia mavazi yao. Timu ya Ivory Coast, inayoongozwa na Jean Louis Gasset, iliwasili ikiwa na mchanganyiko wa mitindo ya kisasa na ya kitamaduni.




Timu ya taifa ya Nigeria, Super Eagles pia ilikumbatia mavazi ya kitamaduni ilipowasili nchini Ivory Coast. Timu ya Nigeria hujumuisha vipengele vya urithi wao wa kitamaduni katika vazi lao la kusafiria na kutikisa wakivalia kaftan nyeupe na kijani kidogo na kofia za rangi sawa.

Senegal ni mshindani mwingine mkubwa katika soka la Afrika, mara nyingi huonyesha utambulisho wao wa kitamaduni kupitia mavazi yao. Mabingwa hao walikwenda na mavazi meupe kabisa, ambayo yalikuwa na vivuli vya rangi ya taifa la nchi





## Ila kwa mbinde sana



**YAMOUSSOUKRO, Ivory Coast**

CAMEROON haikuweza kupata ushindi bora dhidi ya Guine ambayo ilicheza kwa dakika 45 ikiwa na wachezaji 10 tu kufuatia kadi nyekundu aliyoipata nahodha wa Guinea Francois Kamano. Cameroon walitanguliwa kwa bao la mapema la Mohamed Bayo.

Na baadae walipata bao lao la kusawazisha muda mfupi baada ya kipindi cha mapumziko Magri alipofunga kwa kichwa mpira wa krosi bora kabisa wa Georges-Kevin Nkoudou.

## Onana akasirika kwa kuwekwa nje

**YAMOUSSOUKRO, Ivory Coast**

KIPA wa Manchester united na timu ya Taifa ya Cameroon Andre Onana alikasirishwa na kitendo cha kutochezeshwa katika mchezo wa kwanza ambapo Cameroon walitupa karata yao ya kwanza dhidi ya Guinea.

Nyota huyo wa Mashetani Wekundu aliichezea klabu yake katika pambano la Ligi Kuu dhidi ya Tottenham Jumapili, na baadae kuelekea Uwanja wa Ndege wa John Lennon huko Liverpool na kupanda ndege kuelekea Ivory Coast ili kuungana na timu yake ya Taifa.

Onana amekuwa na uhusiano mbaya na Song, na hivyo kumfanya arudishwe nyumbani kutoka Kombe la Dunia la 2022. Uamuzi wa kustaafu wa kimataifa ulitenguliwa ili ajiunge na mipango ya AFCON 2024, lakini mtu ambaye amekuwa na wakati mgumu sana Old Trafford sasa analazimika kumshawishi kocha wake mkuu kwamba anapaswa kukabiliana na Senegal Ijumaa.

# Baadhi ya sajili za dirisha dogo zilizokamilika



- Jimmyson Mwanuke —Simba kwenda Mtibwa Sugar
- Erick Mwijage—West Armenia kwenda Geita Gold
- Erick Johora—Geita Gold kwenda Mashujaa
- Mapinduzi Balama—Coastal Union kwenda Mashujaa
- Shaban Chilunda—Simba kwenda KMC
- Meddie Kagere—Singida Fountain Gate kwenda Namungo FC
- Shiza Kichuya—Namungo kwenda JKT Tanzania
- Reliants Lusajo—Namungo kwenda Mashujaa FC
- Boubacar Sarr—Huru kwenda Simba
- Omar Jobe—Zhenis kwenda Simba
- Manu Lobota- FC Lupopo kwenda Ihefu Abubakar Khomeiny—Singida Fountain Gate kwenda Ihefu
- Augustine Okrah—Bechem kwenda Yanga
- Shekhan Ibrahim—JKU kwenda Yanga
- Salehe Karabaka—KVZ kwenda Simba
- Ladack Chasambi—Mtibwa kwenda Simba
- Abdallah Lanso—Mlandege Kwenda Kmc
- Emmanuel Mtumbuka—Stand United kwenda Mashujaa
- Nasoro Kapama—Simba kwenda Mtibwa Sugar
- Franklin Navaro—Tulua kwenda Azam
- Yeison Fuentes—Itagui kwenda Azam
- David Ulomi—Moloka Swallows kwenda Mashujaa Akram Mhina -Kvz kwenda Kmc
- Mohamed Mustapha—El merikh kwenda Azam
- Jacob Benedict—Mbeya Kwanza/ Prisons
- Feisal Mkoko—(huru)/Prisons Abdulkarim Segeja—Copco/Prisons
- Tariq Simba (Geita/Prisons)
- Ally Msengi (Stelenbosch/Prisons)
- Shabani Msala—Ihefu Mtibwa
- Charles Ilanfya—IhefuMtibwa
- Ayoub Semtawa—huruNamungo.
- Joseph—(huru) Yanga





## Kona ya **Urembo**

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Namna ya kuandaa mkoba kwa muonekano mzuri

JE, nitaamuaje begi la aina mbalimbali napaswa kubeba lenye aina mbalimbali za mavazi (mavazi, kurtis, sketi ndefu zilizochapishwa, suti, nguo za juu n.k)? Linapokuja suala la kuchagua begi linalofaa kwa mavazi tofauti, kuna miongozo michache ya jumla unayohitaji. inaweza kufuata:

Fikiria tukio hili: Kwa matukio rasmi au mavazi ya kawaida, chagua clutch au mfuko mdogo wa kifahari. Kwa mavazi ya kawaida au ya kila siku, tote, crossbody, au mkoba unaweza kufaa zaidi.Linganisha mtindo: Ikiwa umevaa vazi la bohemian kama sketi ndefu iliyochapishwa au kurti, mfuko wa hobo mwepesi au mfuko wa ndoo unaweza k usaidia mwonekano huo. Kwa vazi la muundo zaidi kama vile nguo au sehemu ya juu iliyorekebishwa, mkoba ulio na muundo unaweza kufaa zaidi.

Kuratibu rangi: Ingawa si lazima kulinganisha mkoba wako na mavazi yako kikamilifu, kuratibu rangi kunaweza kuboresha mwonekano wako kwa ujumla. Mifuko isiyofungamana na upande wowote kama vile nyeusi, hudhurungi au nyeupe inaweza kufanya kazi vizuri na aina mbalimbali za mavazi, huku rangi ya pop inaweza kuongeza riba kwa mkusanyiko usio na upande wowote.Zingatia saizi: Saizi ya begi yako inapaswa kuambatana na mavazi yako. Mfuko mdogo unaweza kuonekana umepotea na vazi la voluminous, wakati mfuko mkubwa unaweza kuzidi mwonekano mzuri na mdogo.

Utendaji: Mwishowe, fikiria kile utahitaji kubeba. Ikiwa unahitaji kuwa bila mikono, mfuko wa msalaba unaweza kuwa chaguo bora zaidi. Ikiwa umebeba vitu vingi, tote au mfuko mkubwa unaweza kuwa wa vitendo zaidi.

Kwa kuzingatia mambo haya, unaweza kuchagua mfuko ambao sio tu unakidhi mavazi yako bali pia unakidhi mahitaji yako ya vitendo.Chagua mfuko unaofaaKabla ya kuanza kubeba mfuko wa bega, ni muhimu kuchagua mfuko unaofaa mahitaji yako. Mkoba ambao ni mkubwa sana unaweza kuwa mzito na wa shida kubeba, wakati ule mdogo hautatoa nafasi ya kutosha kwa vitu vyako vyote. Kwa hivyo hakikisha unachagua begi ambalo ni kubwa la kutosha kubeba vitu vyako vyote, lakini sio kubwa sana hivi kwamba inakuwa ngumu kubeba.



**1. Rekebisha kamba.**

Kamba ya mfuko wa bega inapaswa kurekebishwa kwa urefu sahihi kwa kubeba vizuri. Ikiwa kamba ni ndefu sana, mfuko unaweza kuning'inia chini kwenye viuno vyako na usifurahie kuvaa. Kwa upande mwingine, ikiwa ukanda ni mfupi sana, begi inaweza kuwa ngumu sana na inaweza kuwa chungu kuvaa. Kwa hivyo rekebisha ukanda kwa urefu ambao unafaa kwa mwili wako.





**2.Vaa mfuko kwenye bega la kulia.**

Ni muhimu kuvaa mfuko wa bega kwenye bega la kulia. Ikiwa una mkono wa kulia, beba begi juu ya bega lako la kushoto na ikiwa una mkono wa kushoto, beba begi kwenye bega lako la kulia. Hii inahakikisha kwamba unaweza kubeba begi kwa urahisi na kwamba huhitaji kusogea bila raha ili kufikia vitu vyako.

**3. Kusambaza uzito**

Wakati wa kubeba mfuko mzito, ni muhimu kusambaza uzito ili kupunguza matatizo kwenye mwili wako. Weka vitu vizito zaidi katikati ya begi na usambaze vitu vyepesi pande zote. Hii inasawazisha uzito na inafanya iwe rahisi kubeba mfuko.

**4.Kuwa muangalifu.**

Weka jicho kwenye begi lako na uwe macho kwa mazingira yako. Beba begi lako karibu na mwili wako na usiliache likining'inia au bila kutunzwa. Hii inaweza kuzuia mtu kuiba begi lako au kuchukua vitu vyako bila wewe kutambua.Kwa kumalizia, kubeba mfuko wa bega inaweza kuwa njia rahisi ya kubeba vitu vyako. Hakikisha kuchagua mfuko sahihi, kurekebisha kamba kwa urefu wa kulia na kuvaa mfuko kwenye bega la kulia. Sambaza uzito sawasawa na uwe macho ili kuzuia begi lako kuibiwa.



Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo Spoti

| Jumatano Januari 17 - 23, 2024 |

## Roma wamtimua Mourinho



**ROMA, Italia**

JANUARI umekuwa mwezi wa tabu katika maisha ya soka ya Kocha Jose Mourinho.

Familia ya FRIEDKIN inayomiliki klabu ya AS Roma imeamua kumfukuza kazi Kocha huyo.

Mourinho aliyekataa ofa ya kuinoa Liverpool siku chache zilizopita ameondolewa kazini baada ya kikosi chake kuchapwa mechi mbili mfululizo.

Roma wamepigwa bao 1-0 na Lazio na kabla ya kuiabishwa kwa mabao 3-1 na AC Milan juzi.

Kiungo wa zamani wa miamba hiyo ya Serie A, Daniele De Rossi (40) raia wa Italia yupo mstari wa mbele kwenye kinyang'anyiro cha kuchukua mikoba ya Mourinho.



# Stars inawezekana

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' Jumatano hii kinashuka dimbani kumenyana na Morocco katika mechi ya michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

Stars inaundwa na damu mchanganyiko wakiwemo wachezaji wanaocheza ligi za ndani, nje huku kukiwa na nyongeza ya nyota wenye asili ya Tanzania ambao wamerudi kuisaidia timu yao.

Timu hizi mbili ziko kwenye madaraja mawili tofauti lakini lolote linaweza kutokea na kuandika historia mpya.

Tayari Msumbiji bado kidogo iwalaze na viatu Misrii baada ya kuongeza kwa mabao 2-1 mpaka dakika za nyongeza ambapo MO Salah akaswazisha kwa penalti, Guinea ya Ikweta ikivimbia Nigeria kwa bao 1-1 na , Cape Verde walivuruga Ghana baada ya kuwachapa mabao 2-1.

Matokeo hayo yameweza kuishangaza Afrika na Dunia kutokana matokeo waliyoyapata dhidi ya vigogo.

Morocco yenye historia nzuri kwenye michuano hiyo it aingia pia kwa tahadhari dhidi ya kina Mbwana Samatta, Simon Msuva, Sospeter Bajana, Aishi Manula ambaye anatarajiwa kuanza langoni leo.

Nyota kina Benn Starkle, Haji Mnoga, M'mombwa, Feisal Salum, Mudathir Yahya wanahitaji kuonyesha uwezo wao ili pia kutafuta malisho mema zaidi.

## Simba yaachana na Baleke, Phiri

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE panga la wachezaji wa Kikataifa limewaangukia nyota Moses Phiri na Jean Baleke.

Taarifa rasmi ya kiwaaga wachezaji hao imetolewa na klabu ya Simba jana usiku.

Tangia asubuhi jana kulikuwa na tetesi za kuachwa kwa wachezaji hao na ikahitimishwa usiku.

Taarifa za awali zinasema Baleke aliyekuwa Simba kwa mkopo amehitajika katika klabu yake ya TP Mazembe huku Phiri akipeana mkono wa kwaheri.

## Everton, Nottingham zapokwa pointi EPL

**LONDON, England**

TIMU ya Everton FC imekatwa alama 10 kwenye msimamo wa Ligi kuu nchini Uingereza EPL.

Hatua hiyo imefanyima baada ya kukutwa na hatia ya kukiuka sheria za FFP.

Hii nimara ya pili kwa Everton msimu huu kupata adhbu ya namna hiyo.

Nottingham Forest pia imekatwa alama 10 kwenye msimamo wa Ligi kuu nchini Uingereza.

Timu hiyo pia imekutwa na kashfa za Finacia Fair Play.



## Huyu Guede ni Hafiz Konkon Pro

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga ikithibitisha kumsajili mshambuliaji Joseph Guede, Rekodi zinamkataa nyota huyo.

Guede ni mchezaji huru tangu Septemba 2023 baada ya kuachana na klabu ya Tuzlaspor inayoshiriki Ligi daraja la pili Nchini Uturuki.

Guede (29) raia wa Ivory Coast amewahi kuchezea pia katika timu ya FAR Rabat ya Morocco kabla ya kupelekwa kwa mkopo katika klabu ya Emirates ya Jumuiya ya falme za Kiarabu ambako alicheza mechi 24 NA kufunga mabao saba. Awali akiwa na FAR Rabat alicheza michezo 56 na kufunga magoli 16.

Nyota huyo ambaye historia yake inaonyesha amechezea timu nyingi lakini kwa msimu mmoja mmoja.


Mara ya mwisho katika timu aliyotoka hajawahi kufunga bao katika mechi nne aliocheza katika msimu mzima wa Ligi. Rekodi zinaonyesha uwezo wake wa kufunga unapungua kila msimu.

Guede anachukua nafasi ya Hafiz Konkon ambaye mpaka anaondoka Yanga amefunga goli moja katika mechi nne ambazo ni moja tu alicheza dakika 75 wakati zingine alitokea benchi wakicheza chini ya dakika 25.

Konkon wakati anasajiljwa na Yanga kutoka Ghana ndio alikuwa mfungaji bora wa Ligi ya kwao.



## Matokeo/ Ratiba Michuano ya AFCON 2023



**MATOKEO**

Burkina Faso 1 Mauritania 0
Algeria 1 Angola 1
Senegal 3 Gambia 0
Tunisia 0 Namibia 1

**MECHI ZA LEO**

Tanzania VS Morocco Saa 11.00 jioni
Congo DR VS Zambia Saa 2.00 Usiku



